

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|---------------------------------------|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa
Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu
na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/
Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi
ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la
Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi
ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi
ya Makamu wa Pili wa Rais/
Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na
Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi,
Maakazi, Maji na Nishati/
Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu
na Mawasiliano/Kuteuliwa na
Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii,
Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo
na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na
Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na
Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |

18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani

35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwhanani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne – Tarehe 27 Oktoba, 2014

(Kikao Kilanza saa 3:00 za asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Mhe. Ali Abdalla Ali) alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kwa mara yangu ya tatu katika maisha yangu kuja mbele hapa. Mara yangu ya kwanza kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuja kula kiapo na mara ya pili baada ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mnadhimu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, chama kikubwa kwa kunipa jukumu la kuweka hati mezani na kusoma mswada kwa maoni ya Kamati ya Biashara, Viwanda na Masomo na leo mara ya tatu kuleta hoja binafsi.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda naomba uniruhusu kuweka hati mezani, kwa niaba ya Baraza lako la Wawakilishi, kutoa maazimio kuhusu Uimarishaji wa Huduma za Afya kwa Wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba, kwa ufupi unawenza kuita Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kuwa na afya, hapana maisha, bila ya kuwa na afya, hapana uhai. Watu wanatafuta afya kwa gharama yoyote.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 22

Kuingizwa Kwa Nguo za “Modo” na “Pedo” na Athari ya Kiutamaduni Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa karne na dahari Zanzibari imekuwa na utamaduni wake wenywewe wa kistaarabu na heshima ambao imetimia katika kila eneo la maisha ya watu ikiwemo mavazi na mitindo ya urembo. Hali hiyo wameishi nayo wazee wetu kwa karne nyingi sana na kujenga utamaduni bora wa heshima na nidhamu ya maisha kwa watu wa rika zote. Hata hivyo, hivi sasa, ustaarabu na heshima hiyo ya mavazi na urembo imeharibiwa na kusababisha mporomoko wa maadili, kutohana na Serikali kuruhusu biashara za nguo zisizo na heshima na mapambo yanayokwenda kinyume na maadili yetu kama vile nguo za kubana miili kwa akina dada na kaka maarufu kama “modo” na “pedo”.

- (a) Kwa kuwa mavazi hayo yamekuwa na athari mbaya kwa utamaduni wa mavazi ya Zanzibar ambayo huzingatia stara na heshima ya mvaaji, kwa nini Serikali isipige marufuku uingizwaji wa nguo za “modo”, “pedo” na zile zenye matangazo na picha za mihadarati kama vile bangi na kadhalika.
- (b) Kwa vile mavazi hayo hayasaidii kustawisha malezi bora ya vijana wetu, kwa nini Serikaili isiweke viwango vya uvaaji staha na heshima kwa vijana wetu kwa vile huo ni wajibu wake wa kikatiba wa kulinda, kuimariswa na kuendeleza utamaduni wa Zanzibar kwa mujibu wa kifungu cha 10 (f) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.
- (c) Kwa nini Serikali inapiga marufuku bidhaa nyengine zenye athari kama vile tindi kali na kadhalika, lakini inachelea kupiga marufuku uingizwaji wa nguo za “modo” na “pedo”, kufanya hivyo si sawa na kuruhusu

utamaduni wa mavazi Zanzibar upotoshwe kwa makusudi na kukiuka wajibu wa Serikali wa kikatiba wa kulinda, kuimarisha na kuendeleza utamaduni huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 22 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Zanzibar kwa karne nyingi zilizopita na hadi leo utamaduni wake ni wa kistaarabu na heshima iliotimia katika maeneo yote ya maisha ya watu ikiwemo mavazi, mitindo na urembo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa kiasi fulani utamaduni huo umeanza kuporomoka kutokana na kuporomoka kwa maadili yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala la upigaji marufuku kwa uingiaji wa baadhi ya nguo zisizo na utamaduni wa maadili yetu ya Kizanzibari. Suluhu pekee ni kwa wazazi wote kushirikiana pamoja na Serikali kuweza kuelimisha vijana wao, kuondokana na mavazi ambayo hayastahiki kuvaliwa.

Mhe. Naibu Spika, nguo hizo alizozitaja Mhe. Mwakilishi, mara nyingi huvaliwa ndani pamoja kanzu na mabaibui tu. Ni vijana walio na mafunzo madogo ya aina gani ya nguo inapaswa kuvaliwa mbele za watu na aina gani ya nguo inapaswa kuvaliwa na mtu peke yake akiwa yuko ndani.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya aina hii hupaswa kutolewa na wazazi nyumbani na haihusiani na upigaji wa marufuku wa uingiaji wa nguo hizo. Mtu asiyе na maadili akikosa kununua nguo hiyo hapa Zanzibar, ataiagizia kwengine inakopatikana. Mafunzo mazuri ni kwamba dawa za kulevyя zimepigwa marufuku, lakini bado vijana wasio na maadili, huzitafuta mahali popote pale na kuweza kuzitumia.

Kwa upande wa mavazi, kimsingi Zanzibar kuna sheria iliyotajwa ya Kuhifadhi Utamaduni wa Taifa Nambari 1 ya 1973 inayodhibiti maswala ya mavazi. Kama nilivyoleza awali, sheria hiyo kwa sasa inashindikana kutekelezwa kutokana na adhabu zilizomo kama vile utumiaji wa adhabu ya bakora, ambayo inakiuka Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa Ibara ya 13(3), pamoja na kwenda kinyume na haki za binaadamu. Naomba ikumbukwe kuwa adhabu ya bakora ilifutwa rasmi na Baraza lako tukufu kwa mujibu wa Sheria Nambari 6 ya 2004.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, wizara yangu inatafuta uwezekano wa kuirekebisha sheria hiyo ya kuhifadhi utamaduni wa Taifa na tayari wizara inashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuipitia na kutoa ushauri ili hatimae kuifanyia marekebisho na iweze kutumika, ili kuyadhibiti yale yote yaliyoulizwa na Mjumbe kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutokua na afya au nafikiri hajafahamu swali langu la msingi. Naweza kumwambia kwamba sio kweli kwamba nguo hizi zinavaliwa ndani ya mabaibui.

Cha msingi alichokusudia ni suruali za kubana, yaani mtu anavaa anakuwa kama alivyoziwa vile, umbo lake lote linaonekana. Kwa nini nguo hizo hazipigwi marufuku na zinakwenda kinyume na maadili ya Mzanzibari. Hilo la kwanza.

La pili, hata kama zikipigwa marufuku, lini kama mtu ataingiza hizo atakuwa ametenda kosa? Ni lini sheria italetwa hapa Barazani kujadili na kumuacha Mhe. Abubakar, peke yake kutumia vyombo ili kuwe na sheria maalum.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Mwakilishi, nataka nikuambie kwamba kipindi cha mwaka 2012 swali hili liliulizwa Barazani na tulilitolea ufanuzi wa kutosha. Lakini unasema kuwa swali lako sivyo nilivyolijbu.

Swali lako nakuhakikishia ndivyo nilivyokujibu na ninakuambia hivi Mhe. Mwakilishi, kama nilivyoeleza kwenye swalii mama, kuwa tunashirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuileta sheria hii Barazani. Kama nilivyoeleza sheria ya mwaka 1973.

Mhe. Naibu Spika, kama tutaifuata hii hii, basi itatubana wote sisi Waheshimiwa pamoja na watoto wetu na Wazanzibari kwa ujumla.

Mhe. Shadya Mohammed Suleimani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swalii moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, je, wizara yako ina mpango gani wa kutengeneza vipindi maalum vya mavazi pamoja na elimu ya mila na utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi. kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na bodi ya sanaa inatoa vipindi kuelimisha jamii. Hata tulipofanya tamasha Mangapwani, kulikuwa na mitindo mbali mbali ya mavazi yalioneshwa, mgeni rasmi alikuwa ni Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Sasa hivi kwenye bodi ya sanaa wametoa kanda maalum ya kufundisha jamii kuhusu adabu za kula, mavazi na adabu ambazo wanaweza kukaa vijana wetu pamoja na wazazi wao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipatia fursa ya kuuliza swalii moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa sekta ya utalii ni kishawishi kikubwa kinachopelekea vijana wetu kuiga kuvaahizi nguo za vimini, pamoja na *skin tight trousers* na mambo mengine. Sasa kwa kuwa wenzenetu wa UAE, hususan Saud Arabia wanao watalii, lakini wameewewekeea masharti watalii wale kuhusu mavazi pale wanapoingia katika nchi yao.

(a).Je, ni lini Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na askari wetu hapa, Dkt. Shein, itatunga sheria maalum kwa ajili ya watalii, kudhibiti haya mambo ya kwenda nusu uchi katika nchi hii.

(b).Kwa kuwa marehemu mzee Abeid Aman Karume, alimudu kupiga marufuku chupa, yaani zile suruali za chupa pamoja na mabuga walizokuwa wakivaa akina baba. Kwa mfano mzee Jumbe aliwahi kupiga marufuku mabuga, wala alikuwa hawapigi watu bakora.

Je, ni lini Serikali hii kwa namna inayoongozwa na Dkt. Shein, itatunga sheria ya kuweza kuweka masharti ya mavazi au kutunga sheria itakayoweka adhabu, yaani *alternative punishment rather than corporal punishment*, yaani kuweka adhabu badala ya bakora, ili kuweza kudhibiti haya mavazi ya kijinga jinga katika nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nyote kwa ujumla nataka niwaambie hivi, utalii una hasara zake na utalii una faida zake.

Mhe. Mwakilishi, nataka nikuambie kwamba utalii ni jinsi gani wananchi watakavyoupokea na ni jinsi gani wananchi watakavyouona ule utalii ulivyo. Lakini utalii ni mtu mwenyewe binafsi kwa pale maeneo ambayo upo utalii. Kwa sababu tunajua kwamba utalii wanakuja wageni mbali mbali na hawatakiwi, kama nyinyi Wazanzibari wanapokuja wageni muweze kuonesha maadili ambayo hayastahiki, nyinyi wenywewe ndio mnatakiwa mvae vizuri ili wanapokuja watalii na nyinyi waweze kuwaiga mavazi yenu mnayovaa.

Mhe. Naibu Spika, swalii lake la pili, kuhusu sheria. Nimeeleza kwa kina kuhusu sheria yetu ambayo inayohusiana na mavazi. Nilisema kwenye swalii mama kwamba sheria ambayo ilikuwepo ya mwaka 1973, kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu tutaifanyia marekebisho tuilete Barazani, ili muweze kuichangia nyinyi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuweza kutoa maoni yenu na vipengele mbali mbali kuweza kuvikosoa, ili kuingiza vipengele ambavyo vinastahiki kuingia kwenye sheria hii.

Nam. 61

Kukosekana kwa Taarifa za moja kwa moja za Ujenzi wa Meli Mpya

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Usafiri wa baharini ni muhimu sana kwa nchi zote za visiwa ikiwemo Zanzibar, kwa kuwa kwa kipindi kirefu Zanzibar imekuwa ikitegemea vyombo nya kampuni binafsi, kwa ajili ya usafiri wa Unguja na Pemba.

Hivi karibuni Serikali ilitoa taarifa kuwa, imeanza hatua za utengenezaji wa meli mpya ya mizigo na abiria, ambayo taarifa ya mwisho iliyotolewa hapa Barazani ni kuwa meli hiyo ipo katika hatua za kuwekwa mkuku *steel-laying process*. Kwa kuwa SMZ ilipokuwa ikitengeneza meli ya *MV Mapinduzi* katika miaka ya 1970s, ilikuwa shughuli yote ya ujenzi wa meli ile ikioneshwa kupitia televisheni ya Serikali ya mwanzo kuwa ya rangi Afrika ya Kusini mwa jangwa la Sahara ni *TVZ* kwa sasa *TBC-TV*.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea ujenzi wa meli ya sasa unaoendelea utolewe maelezo ya mdomo tu, wakati bado televisheni yetu pendwa ya *ZBC*, yaani zamani ikiitwa *TVZ* inaendelea kufanyakazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 61 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wizara ilikuwa ikitoa maelezo kuhusiana na shughuli za ujenzi wa meli ya Serikali, kwa kuzingatia kuwa kwa kipindi chote hicho kazi zilizokuwa zikifanywa zaidi ni ufanisi na uandaaji wa michoro ya meli hiyo na uthibitisho, yaani *design approval process*, pamoja na uzinduzi wa kazi za ulazaji wa mkuku ambazo kikawaida huzinduliwa rasmi kabla ya kuanza kwa ujenzi wa meli husika.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo mara baada ya kuanza kwa kazi ya ujenzi wa meli hiyo, mnamo mwezi Januari mwaka 2014, baada ya kuzinduliwa rasmi kazi za ulazaji wa mkuku. Wizara imemuagiza msimamizi wa ujenzi wa meli hiyo kampuni ya *STX Marine* ya Korea ya Kusini, kwa kushirikiana na kampuni ya ujenzi wa meli hiyo kuandaa picha za video kwa matukio yote muhimu ya ujenzi wa meli hiyo. Kwa kuanzia na hatua ya utiaji saini, kazi ya ukataji wa chuma, ulazaji wa mkuku. Hadi kukamilika kwa kazi ya ujenzi na kushushwa baharini kwa meli hiyo.

Mhe. Naibu Spika, wizara inatarajia kuanza kuonesha rasmi shughuli za ujenzi huo katika televisheni kwa kuandaa vipindi maalum vya maendeleo ya ujenzi wa meli hiyo, ifikapo mwishoni mwa mwezi wa Disemba mwaka 2014, mara tu baada ya kushushwa baharini kwa meli hiyo, ili kuwapatia wananchi taarifa kuhusiana na maelezo ya ujenzi wa meli ilivyofikiwa.

Mhe. Saler Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, mdogo wangu pale Mhe. Issa Gavu. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika kuimarisha utawala bora na uwazi katika matumizi ya fedha za Serikali, wakati wa miaka ya 1970, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati tunajenga meli ya *MV Mapinduzi*, mbali na kupiga picha za video, lakini tangu hatua ile ya awali ya michoro, ramani na kadhalika ilikuwa hata mlipa kodi wa kawaida anayeishi katika Kijiji cha Vitongoji Umangani pale, pamoja na Ditia walikuwa wakiona hatua ya mchoro ule kwa kupitia chombo chao cha Serikali hiki cha *TVZ*, wakati sasa mnaita *ZBC TV*.

(a) Je, kwa sasa ni sababu gani za msingi zilizofanya ikawa ni siri kubwa mpaka baadae papigwe picha, halafu ndio turushiwe hadi katika *steel-laying*, kwamba ndio walipa kodi wa nchi hii hawajaona kwa kupitia chombo hiki hiki kilichoasisiwa na mzee Karume, ambacho kilikuwa kikituonesha siku zile ujenzi wa *MV Mapinduzi*. Ni siri gani iliopo hadi leo hii kwamba hatujaoneshwa hata ile hatua ya *steel-laying*.

(b) Mhe. Naibu Spika, mbali na kuwa kipindi kile tunaoneshwa kwa kupitia televisheni yetu ya *TVZ* hatua kwa hatua, lakini waziri aliyekuwa na dhamana ya mambo ya mawasiliano na uchukuzi kwa kipindi kile, marehemu Pili Khamis alikuwa akifuatana na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, kwenda kuona kila hatua japo wawili au watatu, wanaona kila hatua inayofikia ya uchongaji wa meli ile ya *MV Mapinduzi*.

- (c) Je, ni lini Serikali yetu hii inayoongozwa na Dkt. Shein hapa, itaweza kupeleka angalau Wajumbe watano wa Baraza hili, nikiwemo mimi mwenyewe ninayeuliza swali hili, ili kwenda kuona hatua kwa hatua ya uchongaji wa meli yetu hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza Mhe. Saleh Nassor, ameleeza kwamba sababu zipi za msingi zilizoifanya Serikali isiwaoneshe wananchi katika hatua zile.

- (a) Majibu ni kwamba katika hatua za kwanza za ujenzi wa meli hii, sehemu kubwa ilikuwa inahitaji uthibitisho wa michoro. Katika hatua kama hii ya uthibitisho wa michoro, sidhani kama kwa mwananchi wa kawaida angelazimika kuionna.

Lakini matarajio yetu ni kwamba hatua ya ujenzi inavyoendelea ndivyo inavyomlazimu mwananchi wetu kuweza kuiona meli namna inavyojengwa na hatua ambazo zimefikiwa. Tumeahidi kwamba Serikali kuanzia mwishoni mwa mwezi wa Disemba mwaka huu tutaonesha kipindi maalum kitakachoonesha maendeleo ya ujenzi huo tokeaa siku ya utiaji wa saini ya mkataba, hatua zilizofikiwa mpaka kukamilika kwa kujengwa kwa meli hii. (*Makofi*)

- (b) Mhe. Naibu Spika, katika mipango ya Serikali katika sherehe zetu zinazotarajiwa kufanyika tarehe 23 mwezi Disemba mwaka huu. Tunatarajia kwamba Serikali itatoa ujumbe maalum kwenda kushuhudia ujenzi na ukamilikaji wa ujengaji wa meli hii huko Mjini Korea ya Kusini.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri wa Miundombini na Mawasiliano, naomba kuulizwa mswali moja la nyongeza lenye vifungu viwili.

- (a) Kwa kuwa utengenezaji meli ni hatua ya kwanza na hatua ya pili ni ushindani wa kibiashara katika soko. Serikali imezingatia vipi fedha ilizotumia kwa ajili ya kununua meli hiyo moja tu, ukilinganisha soko linahitaji kama meli mbili mpaka tatu. Kwanza tukiangalia gharama meli hiyo imetumia kiasi gani, halafu fedha hizo hizo ninachoamini mimi kwamba zingenunua meli tatu mpaka nne kwa fedha hizo hizo tena mpya.
- (b) Chombo huhitaji *services*, kila mwaka meli hupandishwa kwa ajili ya kuangaliwa. Je, itakapopandishwa *dock* meli hiyo Serikali itakwenda kukodi meli wapi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la pili sikulipata vizuri nilikuwa nikiandika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali la pili, taratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri, swali la pili ni kwamba chombo chochote huhitaji huduma ama *services*, sasa kwa fedha hizi imenunuliwa meli moja tu. Je, meli itakapokwenda *services* wananchi wakae wasubiri mpaka irudi, ambapo naamini fedha hizi meli mbili mpaka tatu zingenunuliwa. Je, Serikali itakodi wapi meli au baada ya kuwa meli imapelekwa *dock*, hakuna huduma hizi na Serikali itasitisha huduma hizi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika.

- (a) Gharama za ujenzi wa meli hii ni takribani dola milioni 31.5, ambapo Serikali inenunua na inajenga meli hii kwa azma ya kutoa huduma kwa wananchi wake. Madhumuni makubwa ya Serikali ni kuona kwamba wananchi wake wanaondokana na usumbufu uliopo wa usafiri.

Pamoja na jitihada za wafanyabiashara binafsi katika kusaidia Serikali katika huduma za kuwapatia wasafiri baina ya visiwa vyta Uguju na Pemba, Serikali imeona ipo haja na ulazima wa kuwa na meli yake wenye, ili kuhakikisha wao kama tuna jukumu la msingi la kuwashudumia wananchi tunakuwa na chombo hiki ambacho kitahakikisha huduma za wananchi zinapatikana kutoka katika Serikali yao.

- (b) Swali la pili ni kwamba meli ikenda matengenezo, nini kitakachofanyika. Naamini ni kwamba hivi sasa meli ya Serikali haipo na wananchi wanatasiri. Kwa maana hiyo, meli ya Serikali itakapokwenda kufanyiwa matengenezo bila ya shaka vyombo vivilyopo vitachukua nafasi, kila itakapokuwa meli ya Serikali ipo, huduma zitakuwa zinaimarika zaidi. Hivyo, kwenda matengenezo kwa meli ya Serikali sidhani kama kutaathiri safari kiasi hicho.

Mhe. Naibu Spika, sisi kama Serikali tutalazimika meli hiyo kwenda matengenezo, ili iweze kuishi muda mrefu zaidi kwa ajili ya kutoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Swali la mwisho Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Serikali hii kwa wakati mmoja ilinunua meli tatu mpya MV. Mapinduzi, MV. Maendeleo na hii ya mafuta na zote zilikuwa zinafanya kazi kwa ajili ya biashara na zote hivi sasa ziliopo mbili ziko katika hali mbaya sana na wala hakuna tija inayopatikana katika Serikali isipokuwa ni hasara. Hivyo, meli hii ambayo itagharimu fedha nyingi sana za wananchi na inakwenda kupelekwa katika shirika lile la meli.

- (a) Je, hatuoni kuwa ni kuchukua fedha za wananchi tukazipoteza bure.
- (b) Kwa nini Serikali haioni kuwa iko haja ya kubadilisha mfumo wa kuikabidhi meli hii sehemu ambayo itakuwa ikitia tija.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. waziri, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali iliponunua meli tatu hakukuwa na utandawazi na *liberation* kama ilivyo hivi sasa katika suala zima la biashara huria, kwa sababu kipindi hicho ni Serikali pekee ndio ambayo iliyokuwa ikifanya biashara ya usafirishaji abiria nchini mwetu.

Sasa katika kipindi hichi ambacho tupo tayari kuna mashirika binafsi ya watu wengi, ambayo yanatoa huduma hii ya usafiri kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, Serikali tunalazimika kuwa na meli hii, ili kuhakikisha yaktokea mahitaji ya lazima Serikali tuweze kutoa huduma hii.

Matarajio yetu ni kwamba baada ya kuona changamoto za shirika baada ya kukaa na Serikali kubadilisha mfumo wake, ili kujidesha kibashara, basi tunaaminu kwamba hatua itakayofikiwa shirika hili litaleta tija kwa Serikali na wala haitokuwa upotevu wa fedha kama vile Mhe. Mwakilishi, anavyofikiria.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Katibu tuendelea.

Nam. 52

Tatizo la Maji kwa Wakaazi wa Darajabovu Juu (Uholanzi)

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Maji ni moja kati ya mahitaji muhimu kwa viumbe vyote akiwemo binadamu, kwa kuwa maeneo ya Darajabovu Juu (Uholanzi) ni eneo lenye wakaazi wengi, lakini wenye shida kubwa ya maji, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na katika nyumba za ibada nakadhalika. Kwa kuwa eneo hilo lipo jirani sana na Welezo Pumping Station, ambayo hugawa maji katika maeneo mengi ya Manispaa ya Unguja.

Je, kuendelea kukosa maji kwa wananchi wa Darajabovu Juu (Uholanzi) ni kwa sababu ya Serikali kutowajali wananchi hao au ni uwezo mdogo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuondoa kero za wananchi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 52 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutokubaliana na Mhe. Mwakilishi, kuwa kuendelea kukosa maji kwa wananchi wa Darajabovu Juu (Uholanzi) si kwa sababu ya Serikali kutowajali wananchi hao, kwa sababu Serikali kuititia wizara yangu inaendelea na jitihada mbali mbali katika kutekeleza ahadi ya kuwasambazia wananchi wa mijini na vijijini huhuma ya maji safi na salama.

Ni kweli kuwa katika maeneo ya Darajabovu pamoja na maeneo jirani wanakabiliwa na tatizo la upungufu wa huduma ya maji safi na salama kutokana na kukua kwa mahitaji ya maji ndani ya eneo hilo. Sambamba na ongezeko la makaazi pamoja na uwezo mdogo wa uzalishaji wa kisima kinachotumika kusambazia maji katika maeneo hayo.

Kutokana na hali hiyo wizara yangu kuititia mamlaka ya maji tayari inaendelea na juhudzi za kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo kwa kuchimba kisima katika eneo la Welezo na kukamilika kwa kisima hicho tunategemea kwa tatizo hilo litaondoka la usumbufu wa maji katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, swali la nyongeza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wakaazi wa Darajabovu (Uholanzi) ni walipakodi wa nchi hii sawa sawa na walipakodi wa maeneo mengine ya nchi hii.

Vile vile, wananchi wa Darajabovu (Uholanzi) tangu mwaka 1964 bado *hawaja-enjoy*, yaani hawajanufaika na yale matunda ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar, kwa kuweza kujipatia maji safi na salama katika maeneo yao na badala yake hutumia maji ya kuokota ya hapa na pale, jambo ambalo husababisha madhara makubwa kwa wananchi wa Darajabovu (Uholanzi).

Pamoja na kwamba juhudzi za Serikali tangu mwaka 1964 zinaendelea ili wapate maji watu wa pale Uholanzi. Je, nataka aniambie Mhe. waziri, ni lini? Kwa sababu tangu mwaka 1964 munafanya bidii tu, sasa nataka aniambie kwamba ni lini Serikali itawapatia maji safi na salama walipakodi wale ambao wanalipa kodi zao kwa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. waziri, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lengo na madhumuni ni kuwasambazia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Vile vile, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba maeneo ya Darajabovu tayari tumegundua tatizo, ambalo linasababishwa na uwezo mdogo wa uzalishaji wa kisima chetu.

Kwa hiyo, katika jitihada za Serikali tayari tunachimba kisima chengine ambacho tunaamini baada ya kumalizika kisima hicho basi tatizo hilo la maji ndani ya eneo la Darajabovu litaondoka. Kutokana na hali hiyo, siwezi nitasema nili watatumia huduma hiyo ya maji, lakini baada ya kumalizika kisima hicho basi tatizo hilo nathibitisha kwamba litaondoka katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Asha Bakari Makame, swali la nyongeza.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuhudhuria tena katika kikao hichi kwa hali ya afya njema.

Kwa kuwa kuanzia mwaka 1964, sifirkiri kama mji wa Darajabovu (Uholanzi) watu walikuwa wameshamamia. Kutokana na ongezeko la watu ni kubwa, je, Mhe. waziri, atakubaliana na mimi kwamba si Darajabovu tu wanaokosa maji isipokuwa ni sehemu nyingi ambazo wananchi wanakosa maji. Je, atakubaliana na mimi kwamba

Serikali bado inajitihada za kuhakikisha mule mote ambamo hamufiki maji kwa kuhamiwa kwa wingi yatafikishwa. (*Makofii*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. waziri, majibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika mwaka 1964 eneo la Darajabovu (Uholanzi) mpaka Mtoni yalikuwa ni maeka ya wananchi na wala watu walikuwa hawaishi katika eneo lile. Lakini baadae watu wameongezeka na Serikali inaona umuhimu wa kuhakikisha kwamba watu kila walipo wanapelekewa maji.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwamba kuna kisima kinachimbwa katika mradi wa *Ras-el-Kheima* ambapo tayari kimeshachimbwa, kwa ajili ya kusaidia kupunguza tatizo la maji katika eneo lile na halafu na mambo mengine mengi yanachukuliwa jitihada, ambapo ni pamoja na miradi ya *ADB*, miradi ya *ADF12* pamoja na miradi mingine mbali mbali kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji katika maeneo tofauti. (*Makofii*)

Kuongezeka kwa watu ni kweli kama alivyosema Mhe. Asha Bakari Makame, kunasababisha upungufu wa maji. Kwa mfano unapokwenda katika *mains* ya maji na ukazitoboa zile *mains* na kupeleka maji sehemu nyengine ujue kuna watu umeshawapunguzia maji.

Hata hivyo, wizara yangu inajitahidi kulishughulikia suala hili, ili kuona kwamba kila mtu alipo anapata maji na hiyo ndio jitihada tunayoendelea nayo. Hivyo, tunategemea miradi hii itakapokamilika tatizo hili litakuwa limeondoka kabisa. (*Makofii*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mhe. waziri, swali limechukua muda mrefu. Katibu tunaendelea.

Nam. 50

Maendeleo ya Wafugaji wa Nyuki katika Jimbo la Wawi

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na mambo mengine wamekuwa wakisaidia sana juhudzi za wakulima wa zao la karafuu kwa kuwapatia miche, majamvi, karabai na kadhalika. Katika suala zima la kuongeza kipato pamoja na kupunguza umasikini, vikundi mbali mbali nya akinamama pamoja na vijana wamekeza maisha yao katika ufugaji wa nyuki.

Je, ni mara ngapi wizara imetembelea wafugaji nyuki katika Jimbo la Wawi waliopo Umangani, Vumbe, Matungu, Kibokoni, Makaani na kadhalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 50 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, nyuki ni moja ya mali ya asili ambazo zinashughulikiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa mantiki hiyo wizara inawatambua wafugaji wa nyuki wote na wafanyakazi wake, wanawatembelea mara kwa mara kuititia vikundi nya ndani ya majimbo Unguja na Pemba.

Si wafanyakazi tu bali mimi mwenyewe Naibu Waziri, Waziri pamoja na uongozi mzima wa wizara huwa kwa nyakati tofauti wanawatembelea wafugaji hao Umangani, Kibokoni, Makaani na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, swali la nyongeza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kumpungeza Mhe. Naibu Waziri, kwa ziara zake alizofanya kwa wajasiriamali pamoja na hawa waliowekeza nguvu zao katika ufugaji wa nyuki katika maeneo

ya Umangani mpaka kufikia Kibokoni kule na aliahidi kuchangia chochote ambacho atawapelekeea na naomba kwa hili Mwenyezi Mungu amzidishie na ule mchango aliyosema atachangia kule basi achangie.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ufugaji wa sasa wa nyuki, yaani sasa nyuki hawafugwi katika mapori isipokuwa wanafugwa katika mabanda yaliyokuwa ni *airtight*, yaani wameezekwa vizuri na hayapitishi upepo.

Mhe. Naibu Spika, na kwa kuwa wafugaji wangu pale Umangani wengi na pamoja mpaka Kibokoni kule wanafuga nyuki katika mabanda ambayo yanavuja ya makuti ambayo yanavuja vuja pamoja na juhudu ambazo hupita kusaidia, lakini kidole kimoja hakibanjii chawa.

Je, ni lini Serikali hii yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itawasaidia wafugaji nyuki katika jimbo langu kuititia wizara yako Mhe. Naibu Waziri, kwa kuweza kuwasaidia angalau mabati pamoja na matofali ya kujenga mabanda ya kisasa, ili waweze kuzalisha kwa wingi na walipekodi Serikali na hatimaye hiyo meli ipate kuja haraka kuititia kodi za wananchi hawa wafugaji wa nyuki.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. waziri, majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu tunawapenda sana na naimani kwamba wizara yangu ya kilimo kuititia Serikali jitihada tunayoifanya katika wafuga nyuki ni kuwapatia mambo mengi katika moja ni utaalamu na hilo ni jukumu letu, kuwashajihisha. Lakini suala la kuwapatia uwezekaji wa mabanda ni suala ambalo kwa upande ni kuwapa taaluma kwa sababu wafuga nyuki wameimarika kweli kweli.

Sasa ikiwa jimbo la Mhe. Mjumbe, pamoja na jimbo jengine watataka hayo. Kwa mfano ukizama Unguja kuna wafuga nyuki kila sehemu wapo na Pemba sio jimbo lake tu na kila sehemu wapo. Kwa hivyo, kuchukua ahadi kwamba tutawasaidia mabati na makuti hilo sitoweza kutoa hapa katika hadhara hii, isipokuwa kama Mwakilishi basi tukakae pamoja katika majimbo yetu kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali wetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na mimi kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. waziri, suala la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar azima yake ni kupunguza umasikini kwa wananchi wetu na kwa kuwa wafugaji wa nyuki vikundi hivi vimo sio Chake Chake na Kibokoni tu bali wapo sehemu nyangi sana. Sasa manuuliza Mhe. Waziri, pamoja na kuwa amekiri kwamba utaalamu unatoka katika wizara yao, ni mara ngapi wataalamu wake wanawatembelea wafugaji wa nyuki na kuwaelekeza katika utaalamu.

Je, kwa kuwa ufugaji wa nyuki unahitaji zana na mizinga ya sasa mpaka iundwe, ni mabao yanayoundwa kwa gherama. Je, wizara yake inawasaidia vipi wananchi hawa kupata mizinga zaidi ili wazalishe asali nyangi kuwauzia na kupunguza umasikini kwa wananchi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Mheshimiwa, wizara yangu wataalamu wa nyuki siku zote wanawafuata wakulima wa nyuki ambao wanatengeneza nyuki ili kuwapa mafunzo haya na ukitaka hayo kwa sababu kilimo cha nyuki kimeanza hivi karibuni sio zamani sana, ile kuwattembelea watalaamu na kuona matatizo yao ndio maana wamehamasika na kuongezwa vikundi mbali mbali kila siku vikundi vimejitokeza kuimariika jinsi ya utengenezaji wa nyuki.

Suala la kuwasaidia kuhusu mizinga, mimi mwenyewe binafsi nishawahii kugawa mizinga mia mbili mara ya kwanza, wakaja watu wa Pemba, Kitogani nikaigawa mizinga ile, Kibokoni, Umangani na sehemu nyengine wakachukua mizinga, kila kikundi nakumbuka wakachukua mizinga yao, waliopata mizinga minne, minne na mitano, mitano na juhudu hiyo itaendelea ya kutoa mizinga, ukizingatia mpaka sasa kuna vikundi ambavyo vimenufaika kwa mizinga hiyo kupatiwa mtu mmoja, mmoja, mpaka kwa vikundi kuna jumla ya wafugaji nyuki 538, hawa walipatiwa mizinga wakiwemo wanawake 271 na wanaume 267.

Mhe. Mwajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba jina langu kidogo lirekebishwe naita Mwajuma Faki Mdachi. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri, amekiri kwamba ametembelea sehemu nyingi za Pemba, lakini kwa kuwa Wilaya yangu ya Mkoani viko vikundi hivyo vya ufugaji wa nyuki. Je, nataka Mhe. Naibu Waziri, anieleze ni kikundi gani na kipi ambacho amekitembelea katika Wilaya ya Mkoani. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Mheshimiwa, katika vikundi vya Mkoani vyote vya nyuki bado hatujavitembelea, nilitembelea sana vikundi vya Chake Chake na Wete, lakini namuahidi kwamba vikundi vya Mkoani navyo tumo katika *process* ya kuvitembelea, kwa sababu kama tunavyosema vikundi vya nyuki vimeimarika kwa wingi, kwa hivyo, navyo vya Mkoani tayari tumo katika *process* za kufanya ziara na kuvitembelea.

Nam. 31

Tatizo la Ugonjwa wa Fistula kwa Akina Mama wa Zanzibar

Mhe. Saleh Nassor Juma: -Aliuliza:-

Afya ya mama na mtoto ni suala muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha suala hili imefanya jitihada kubwa ya kujenga vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali za *Cottages* za wilaya, mikoa na imo mbioni kuboresha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa na kwa kuwa hivi karibuni katika nchi za jirani kuna taarifa kuwa baadhi ya akina mama hupata tatizo la kusumbuliwa na uwezo mdogo wa kuzuulia choo kidogo pale wanapojifungua (*fistula*).

- a) Je, tatizo hilo limeshawahi kujitokeza hapa Zanzibar.
- b) Kama limeshawahi kujitokeza ni hatua gani zilichukuliwa na Serikali ili kulizuwia lisiendelee kutokea.

Mheshimiwa Waziri wa Afya Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, swali lake Namba 31 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba tukiri kuwa ni kweli afya ya mama na mtoto ni suala muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote lile, pia, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha suala hili imefanya jitihada za kutosha na kubwa za kujenga vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali za *Cottages* za wilaya, mikoa na hivi sasa imo mbioni kuboresha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa.

Kwa kuwa hivi karibuni katika nchi za jirani kuna taarifa kuwa baadhi ya akina mama hupata tatizo la kusumbuliwa na uwezo mdogo wa kuzuulia choo kidogo pale wanapojifungua, yaani (*fistula*) hili ni kweli tatizo hilo lipo na pia limeshawahi kutokea hapa Zanzibar na tayari hatua kazaa zimeshachukuliwa na Serikali katika kulitatua na kulipatia tiba na kwa kushirikiana na wenzetu Tanzania Bara ambapo tatizo hili ni kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya ziada kabla sijajibu suali la Mheshimiwa Mwakilishi, kwanza kabisa kuvuja kwa choo kidogo baada ya kinamama kujifungua uzazi hutokana na sababu kuu zifuatazo ambazo ni nne:

1. Kwanza kabisa ni uzazi kandamizi, yaani *extracted labour*, mtoto kuwa mkubwa na kichwa cha mtoto kukandamiza chini katika njia ya uzazi ambapo hapo hapo chini yake kuna njia ya kutolea mkojo;
2. *Prolong second stage labour*, yaani ule uchungu wa mama mzazi kuchukua muda mrefu zaidi kwa stage ya pili ambapo hutokana na mtoto kukaa katika eneo lile lile aka-*apply pressure* kubwa na njia ile kupasuka;

- 3). Ni *distance between the hospital au deliver replace* na nyumbani kwa mama, yaani masafa kuwa marefu kwa hapa Zanzibar, hatuna tatizo hilo kwa sababu vituo vyote vya afya viko chini ya kilomita tano, lakini wenzetu Bara hilo linawatatiza sana kwa sababu unakuta wakati mwengine hospitali iliyokuwa karibu ni kilomita hamsini au mia. Sasa na lile pia ni tatizo la *delay* huwa linasababisha tatizo hili la *fistula*.
- 4). Na mara nyingi madaktari katika sehemu ya nne huwa wanaita *PPP*, yaani P tatu ya kwanza ni *passenger*, yaani mtoto mwenyewe. P ya pili ni *passage*, yaani njia ya kutokea na P ya tatu ni *power*, yaani ndio lile la nne nililokuwa nalisema kwamba mama mzazi kuwa na nguvu na pumzi za kumsukuma mtoto ili atoke kwa wakati na asikae kwenye lile eneo ambalo mtoto huwa ameshakaa katika njia ya kutokea.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi, kuwa ni kweli tatizo hili la kusumbuliwa na uwezo mdogo wa kuzuia choo kidogo pale wanapojifungua kina mama lipo na mara nyingi hutokea kutokana na sababu hizo nilizozitaja na husababisha kupasuka kwa njia ya kibofu cha mkojo ambayo husababisha *fistula* ya kibovu cha mkojo na sehemu ya ukeli, yaani *recto vaginal fistula*.

Mhe. Naibu Spika, wizara kupitia kitengo shirikishi cha afya ya uzazi na mtoto ikishirikiana na madaktari bingwa kutoka *CCBRT* Msasani Dar es Salaam, wamechukua hatua za kuelimisha kwa kupitia katika vituo vyote vya afya Unguja na Pemba na kutoa taarifa ya matatizo haya kupitia radio na televisheni, ambayo matangazo haya yanændelea kutolewa ili kutoa elimu kwa wananchi. Huduma za uzazi pia zimesogezwa kwa wananchi karibu zaidi ili kuzuia lile tatizo la *delayed labar*.

La tatu, tunatoa elimu kwa madaktari wetu kutokana na matatizo haya ya *fistula* ambayo madaktari kadhaa wameshakwenda pia kupata semina mbali mbali ya jinsi ya kutatua matatizo haya.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wanapata matatizo haya huwa wanapatiwa matibabu katika kituo cha afya cha karibu yake na kisha mgonjwa huyo huletwa kwenye kitengo cha afya ya uzazi na mtoto na ikibidi basi hufanyiwa taratibu ya safari kuelekea *CCBRT* Msasani Dar es Salaam ambapo matatizo haya huwa yanashughulikiwa kwa upana zaidi kwa ajili ya matibabu zaidi. Matibabu na safari ya mgonjwa huyo hugharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wote kuwa wafike hospitali mapema mara tu, hasa akina mama watakajigundua na tatizo hili la *fistula* ili mgonjwa apatiwe matibabu yaliyo sahihi na haraka, huduma hizo kwa hivi sasa kwa hapa Zanzibar hutolewa katika *cottages* za hospitali zote ikiwemo ya Makunduchi, Kivunge, Mwembeladu, Chukwani ndani ya jimbo la Kiembesamaki, na Fuoni na vituo vyengine vimo njiani vinatayarishwa katika ile orodha tuliyosema, vituo 22 vinavyotengenezwa ili viweze kutoa huduma hiyo.

Kwa upande wa Pemba huduma hizo hutolewa Wete, Chake Chake, Mkoani, Micheweni na Vitongoji Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana sio tu kwangu mimi ninayejibiwa, lakini hata kwa walipo kodi huko nje ambao wametoa taaluma nzuri, aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa *fistula* ni ugonjwa unaowapata akina mama na kwa kuwa akinamama ni watu wa haya sana na wanaona aibu na kwa aina zote za *fistula*, yaani *radical, black fistula*, sijui *remary fistula*, zote zinasababisha aibu na taharuki kubwa kwa mama zetu na kwa kuwa tiba yake inahitaji sana taaluma, yaani kwanza kabla ya kutiwiwa unahitaji upate taaluma sana na taaluma zinatolewa katika vituo vya afya ambavyo akina mama wengi hawendi hata kupima ujauzito na kupata huduma za kiafaya kama mama na mtoto kule katika vituo.

Je, kwenda kupata taaluma huko si itakuwa tabu zaidi, sasa naomba Mhe. waziri, anijibu ni lini wizara yako itafanya *mobile education training* vijijini huko ili kuenda kuwaelimisha kwa kushirikiana na sheha wetu pamoja na madiwani? Ni lini watapita vijijini Wizara yako ya Afya na wataalamu wake kutoa mafunzo kwa wakina mama hasa hawa wa vijijini ambao wana tabu sana kwenda kwenye *clinic* kwenda kupata hii elimu ya uzazi wa afya ya mama

na mtoto? Ni lini wizara yako itapeleka elimu hii vijiji? Sio pale hospitali na kwenye vituo vya afya tu, lakini vijiji ni lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwanza naomba nipokee mawazo yake mazuri hususan haya ya *mobile education* ya kwenda vijiji na hivi juzi tumepokea baadhi ya vifaa na pia, yakiwemo magari ambayo yatatumika kama *ambulance*, lakini zile sio *complete unites za ambulance*, ila ni *semi* kati ya kutoa huduma na kufikisha mgongwa mapema hospitali, pia kuna magari yale ambayo tulipata msaada kutoka *UNESCO* kwa ajili ya kutolea elimu mbali mbali kwa jamii. Pia, nahisi mawazo haya ni mazuri sana kutumika katika kutoa elimu kwa kinamama.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, la muhimu sana ninachofaidika hapa ni *cancelling*, yaani ushauri nasaha kwa yule mwanamama au mwanamke kumshauri mpaka akubali kuja, kwa sababu elimu wanajua kupitia matangazo ambayo yanatoka kwenye TV, lakini ni ile haya na aibu aliyoumbwa nayo mwanamke baada ya kujitokeza kwamba tatizo lile analo, mara nyingi tatizo hili wanawake huwa hawajitokezi linagundulika kutokana na harufu ambayo hutokana na yale mazingira ya kutokwa na haja ndogo au haja kubwa katika *rectal* au *renal fistula*.

Sasa muhimu zaidi nguvu tunataka tuzielekeze kwenye *house ling* na hii iwe *one by one*, yaani mtu mmoja kwa mmoja huwezi kwenye hadhara ya kinamama wengi au kwenye *mobile education* mwanamke ajitokeze kusema mimi ninalo hili tatizo, kwa hivyo kitengo cha ushauri nasaha kipo na sisi tutaendelea kushajihisha kama wizara ili wanawake waweze kupatiwa ushauri nasaha mpaka huko vijiji, yaani kushauri na kubembeleza mpaka alikubali kwamba hili tatizo ninalo ili aweze kufika kituo cha afya. Mara nyingi kina mama huwa hawajitokezi kufika kituo cha afya wanapokuwa na tatizo kama hili. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja la nyongeza. Lakini kabla ya kuuliza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kina kama vile ni mtaalam wa fani hii ya afya.

Mhe. Naibu Spika, nimeelezwa hapa kuwa haya maradhi haya ya fistula yanababishwa na mambo manne makubwa, ambalo moja katika manne ni masafa kuwa marefu kwa sisi yametuondokea, lakini ninavyojua mama anapoanza kuwa mja mzito huwa anakwenda katika vituo vya afya husika na kupia afya yake, wanaopima ni wataalam na wanamjua mama alivyo wanamjua mtoto alivyo, wanamjua lini atazaliwa kuwa ni mwanamke au mwanamume.

- a) Je, katika kupima ikionekana kuwa kuna hatari ya mama huyu baada ya kujifungua kupata maradhi haya hakuna taaluma inayoweza kutolewa kwa mama huyu kabla ili mambo haya yasitokee wakati anapokwenda kupima afya yake.
- b) Kwa sababu Tanzania bara kuna taasisi inatibu maradhi haya bure kwa nini Mheshimiwa Waziri haoni kuwa kuna umuhimu na Zanzibar pia kuombwa wale wakaja kuwatibu watu hawa wakati wapo na tukaepukana na Serikali kutumia fedha nyingi kwa matibabu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwanza nashukuru sana kwa kutoa maeleo ya kwamba masafa ni marefu wakati mwengine husabisha matatizo kama haya, ila kupima kwa afya ya mama kwenye hizi *clinic* ni muhimu na nashukuru kina mama wanajitokeza kwa wakati kupima afya na mara nyingi pia huwa wanashauriwa hususan pale mtoto anapokuwa mkubwa kuliko umbile au umbo la mwanamke, huwa anashauriwa kwamba huyu mtoto ni mkubwa na tarehe zako zitakuwa fulani ambazo unategemea kupata huyu mtoto.

Pia, ushauri wa pili wanaopewa ni kwamba, je, atafanya *normal delivery*, yaani atazaliwa kwa kawaida au atahitaji *caesarean section*, yaani kupasuliwa kwa kuzalishwa yule mtoto, ushauri huo huwa unatolewa

La tatu, anapangiwa kituo ambacho atapata huduma ile kama ni kituo cha karibu na kwake au hospitali kubwa zenyet vifaa vingi zaidi vya kututua matatizo kama kutakuwa na matatizo katika ukubwa wa mtoto wakati wa kuzaa, kwa hivyo, hayo yote Mhe. Naibu Spika, yanafanyika ila kinachotakiwa kushajihisha zaidi, sasa hivi ni kwamba hayo matatizo yanapogundulikana tu mapema kabisa basi yule mwanamke aweze kupatiwa zile huduma na kuwa

karibu zaidi na hospitali ili asiwe masafa mrefu. Yaani hata kama kulazwa inabidi alazwe, basi aanze kupatiwa *admission au bed rest* katika kipindi hicho cha kujifungua kwake ili asiwe mbali na huduma za hospitali.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili, kuja hawa wataalamu hapa Zanzibar, hapa Zanzibar hizi *operations za fistula*, yaani kufunga njia ya mkojo ambayo imepasuka kutokana na uzito wa mtoto au *pressure* kuwa kubwa zinafanyika, isipokuwa sio kwa wingi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wenzetu wanafanya *operation* kama hizi nyingi zaidi kwa siku, wao wana vifaa vingi zaidi na utaalamu mkubwa zaidi. Hapa ni *very rare cases*. Kwao wao inatokea kwa wingi zaidi kutokana na masafa yao ni mrefu zaidi. Mfano kama kule Dodoma kutoka Gairo mpaka kuja Dodoma Mjini, takriban kilomita 80 mpaka 90, kwa hiyo, muda wa masafa huwa mrefu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa Afrika, nchi ambayo imekubwa na matatizo makubwa sana ya *fistula* ni Ethiopia, ndiyo inayoongoza. Nayu pia ni kutokana na masafa kuwa mrefu, sio jengine lolote, wala sio ukubwa wa mtoto kwa kule nchini Ethiopia, lakini ni masafa kuwa mrefu.

Mhe. Naibu Spika, mimi namshukuru Mhe. Mwakilishi kwamba wazo ni zuri ila mambo kama haya huwezi kufanya *camp* kama ile ya macho au kadhalika. Kwa sababu hujui mama atazaa lini au mimba ile itaingia lini au mtoto atapati kana lini. Isipokuwa watakapokuja hawa wataalamu tunaweza kuwaomba pia kufunga kitengo kama hiki cha *CCBRT* au *extension ya branch* yao kwa hapa Zanzibar ambayo itaendelea kutoa huduma zile zinazofadhiliwa na Serikali ya Watu wa Ujerumani. Ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya, suali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza suali la nyongeza nilikuwa naomba tu kwamba *sometime* masuali ambayo yanatuhusu sisi kina mama ni vyema ukatupa nafasi sisi wenye ali kuyauliza. Kwa sababu hasa ukizingatia ule msemo unaosema kwamba "anayevaa kiyatu ndiye anayejua wapi kinamfinya".

Mhe. Naibu Spika, baada ya ufanuzi huo naomba kumuuliza Mhe. Waziri, suali moja la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri, katika majibu yake amesema kwamba hospitali ya *CCBRT* inatoa huduma na amesema kwamba SMZ hugharamia *cost* za matibabu hayo. Lakini mimi kama balozi wa *fistula* nafahamu kwamba *CCBRT* ikishirikiana na *Vodacom* wanatoa matibabu haya kwa akina mama bure kabisa ikiwemo usafiri, malazi na matibabu yenye ali.

- a) Mhe. Naibu Spika, nataka kujuu ni akina mama wangapi kutoka Zanzibar wamepata huduma hii ambayo inatolewa *CCBRT* na *Vodacom*, ukiachia mbali ile ambayo ya SMZ inagharamia.
- b) Mhe. Naibu Spika, nimesikiliza vizuri maelezo ya Mhe. Naibu Waziri, wakati anajibu hili suali sikuona sehemu ambayo ameleeza kwa hapa kwetu, hili tatizo ni kubwa kiasi gani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba aeleze kwamba *how big the problem* hapa kwetu.

Mhe. Naibu Spika: Naomba Mjumbe nikufahamishe kwamba uzazi ni baba na mama na sisi tunaambiwa tuwashauri kina mama, kwa hivyo, hatufanyi vibaya, Mhe. Waziri, majibu. (*Makofifi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa majibu yako wewe pia mazuri sana, ambayo umetoa katika kufafanua kazi zinazofanywa na Wizara ya Afya.

- 1) Mhe. Naibu Spika, hapo awali nilishasema kwamba huduma zinazoghamiwa na Wizara ya Afya ni huduma za usafiri, mara nyingi hutolewa tiketi ya boti na labda kama kuna msindikizaji na ye ye husaidiwa kwa kwenda Dar-es-Salaam na kurudi. Sisi tuna mashirikiano ya karibu sana na *CCBRT* na hakuna gharama zozote kule za tiba. Mbali ya hao *Vodacom* na hata hao *CCBRT* wenye ali wana *sponsorship* yao ya maradhi haya ya *fist* ambapo sisi huwa hatulipi chohote.

Sikusema kwamba mgonjwa anapaswa kulpia au Wizara ya Afya inalipia. Tunacholipia sisi au kugharamia ni huduma za usafiri, hilo la kwanza.

- 2) Mhe. Naibu Spika, pia, alizungumza katika utangulizi wake kwamba mambo ya akina mama wanapenda wenyewe yawe yanazungumzwa *in private* kwamba katika faragha zaidi na ni kweli mimi hapa nimekuja na mambo mengi kidogo hata baadhi ya picha ninazo hapa ni nzuri za kuonesha mambo mazuri, lakini nimeshindwa kuzitoa kwa sababu bado utamaduni wetu hauturuhusu.

Mhe. Naibu Spika, katika hilo ulilolisema wewe na Wizara ya Afya hivi sasa kupitia vituo vyote na wana taaluma wake wote hata mama anapokwenda kwenye *clinic* basi afatane naye baba waende pamoja. Kwa sababu lile ni suala lao wote wawili. Baba anapokuwa pamoja na mwana mama au mwanamke anapokwenda kwenye *clinic* ya kwenda kupima uzazi, basi yule mwanamke anapata faraja kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia, kuna uthibitisho wa kisayansi kwamba baba amapokuwa na mwanamke mpaka dakika ya mwisho ya *labor* mpaka wakati wa uchungu basi ule uchungu anakuwa mwepesi zaidi anapokuwepo baba na mama pamoja. Kuna uthibitisho huo kuliko mama akiwa ameachwa peke yake.

Mhe. Naibu Spika, utamaduni huo tayari umeshaanza na tunaendelea kuelimisha na naomba Waheshimiwa Wawakilishi, waendelee kuwashajihisha hususan kina mama kutoa elimu zaidi kufuatana na waume zao wakati wanakwenda kuanzia kupima mimba mpaka wakati wa kuzaliwa mtoto, mwanamme ashiriki kikamilifu katika *the labor process*.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa kama nilivyosema hapa awali kwa Zanzibar tatizo hili si kubwa kwa sababu tatizo lile la *distance* halipo, yaani masafa kuwa marefu kati ya vituo. Tatizo la kina mama kuwa na nguvu ya kuzaa halipo. Tatizo lilokuwepo hapa Zanzibar ni dogo sana, mtoto kuwa mkubwa kuliko umbile la mwanamke.

Mhe. Naibu Spika, mara nyangi Mungu ametujaalia bahati sisi akina mama wetu wana afya nzuri zaidi na hiyo kwa kuwa tumetokana na mwambao wa pwani naamini wanakula samaki, pweza, ngisi, vile vyakula vyenye virutubisha zaidi ndani ya mwili na ndio maana mtoto anakuwa kuliko umbile la mwanamke, hususan akina mama wafupi, mtoto anakuwa mkubwa zaidi. Sasa pale ndio mara nyangi matatizo haya hutokeea.

Mhe. Naibu Spika, kwa takwimu za wastani Zanzibar tunapata kati ya wagonjwa wawili mpaka watatu wenye tatizo kama hili kwa mwezi ambao huwa wanapelekwa Dar-es-Salaam na hawafanyiwi hapa *operation* zile wawili au watatu, kwa sababu inakuwa ni ngumu zaidi unapokuwa huna *mass* kubwa ya kufanyiwa *operation* hiyo kutokana na vifaa vyake vinavyohitajika katika *operation* hiyo, ni vifaa vidogo sana. Kwa hiyo, hao tunawahudumia kwa kuwapeleka Dar-es-Salaam. Tatizo hili si kubwa, kwa hiyo, wastani wake ni kati ya wagonjwa wawili mpaka watatu kwa mwezi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Saleh Nassor Juma, suali linalofuata.

Nam. 32

Tofauti za Ugonjwa wa Kisukari wa Kawaida na wa Kikojozi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Tatizo la kiafya la mwanadamu kwenda haja ndogo mara kwa mara inasadikiwa kuwa moja ya dalili za ugonjwa wa sukari (*diabetic melitus*). Aidha, kuna taarifa za kitaalamu kwamba tatizo kama hilo husababishwa na uwezo mdogo wa mwili wa binaadamu kushindwa kutengeneza kichchoeo cha mwili, yaani *hormone* anayeyitwa "*anti-diuretic hormone*" (*ADH*) na hivyo husababisha ugonjwa unaoitwa "*diabetic insipidus*"

- a) Je, maelezo haya ni ya kweli.
- b) Kama ni ya kweli ni tafauti gani iliyopo baina ya ugonjwa wa sukari wa kawaida (*diabetic mellitus*) na huu wa kikojozi (*diabet insipidus*).
- c) Kwa kuwa tiba ya ugonjwa wa sukari ya kawaida unajulikana, je, tiba ya ugonjwa huu wa "*diabetic insipidus*" ipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma, suali lake Nam. 32 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- a) Kwanza kabisa naomba tukiri kwamba kwa kweli maradhi yaitwayo "*diabetes insipidus*" yapo, nayo husababishwa kutokana na *hormone* ama (kichocheo cha mwili) kinachoitwa "*anti-diuretic hormone*" na zipo tofauti kadhaa kati ya *diabetes mellitus* na *diabetes insipidus*.
- b) Mhe. Spika, tofauti kati ya *diabetes mellitus* na *diabetic insipidus*.
 - i. *diabetes mellitus* ama inajulikana hii ni sukari ya kawaida, inasababishwa na upungufu wa kukosekana kwa *hormone* aina ya *insulin* inayotolewa na kongosho (*pancrease*). Hili jina la kongosho hata mimi nilikuwa nalisikia kwa kiswahili mara ya kwanza, lakini najua kuna *pancrease* kwa kiingereza. Wakati *diabetic insipidus* inasababishwa na kukosekana kwa *hormone* aina ya *anti-diuretic* inayotolewa na sehemu ya ubongo ambayo ipo chini ya ubongo (*pituitary gland*).
 - ii. Mhe. Naibu Spika, tofauti nyengine ni *diabetes mellitus*, sukari huwa inapanda panda sana kwenye damu wakati *diabetes insipidus* sukari inakuwa ya kawaida kwenye damu na ile hisia ya ile *hormone* katika mkojo inakuwa kubwa zaidi na inakuja kwa haraka na ndio maana mganjwa mwenye *insipidus* huwa anatokwa na mkojo kwa haraka kabla ya kuwahi kufika kwenda kujisaidia.
 - iii. Mhe. Naibu Spika, *diabetes insipidus* mwili huwa unapoteza maji kwa haraka sana, yaani maji ya mwili huwa yanatoka haraka sana.
- c) Tiba ya ugonjwa huu ya *diabetic insipidus* ipo ambayo ni kumpatia mganjwa *anti-diuretic hormone* ambayo haitolewi na hiyo *pituitary gland* ambapo anaweza kupewa kwa kunusa na hiyo dawa ya kunusa inaitwa *desmopressin hormone*. Wagonjwa kama hawa ni wachache mno, naweza kusema ni mmoja labda kwa mwaka ambaye anaonekana katika vituo vya afya.

Mhe, Naibu Spika, mara nyingi hapa Zanzibar madaktari wetu huwa wanatibu wagonjwa hawa kwa kuwapa hiyo *anti-diuretic hormone* ambayo zipo, lakini kutokana na uchache wao basi mara nyingi inakuwa haitajiki tiba hiyo.

Mhe. Naibu Spika, ila *diabetic mellitus*, wagonjwa hawa ni wengi. *Diabetic mellitus*, kama nilivyosema ni kongosho na *insulin*. Lakini pia, inatokana na vyakula tunavyokula vya sukari vingi na kadhalika. Ambapo hii *diabetic insipidus* haisababishwi na mwenendo wa maisha, kukosa mazoezi, uzito kuwa mkubwa na kula vyakula vyenye sukari au *starch* kwa wingi sana kupita kiasi. Nashukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya suali langu hili aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, kitaalamu kabisa naomba nimuulize suali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa hii tiba ya *diabetic mellitus*, ambayo husababishwa na *hyperglycemic fat* katika damu, ipo na tunaipata na hii ya *diabetic insipidus* ni ya kunusa ambayo sijawahi kuiyona hata siku moja.

- a) Je, huyu *hormone* unayemnusa na kutibu hii *diabetic insipidus hormone* ni tiba ya kudumu hii.
- b) Je, kupitia watalamu wako Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu huyu *hormone, anti-diuretic hormone*...anatolewa katika ubongo na *inasadikiwa anatolewa katika posterior lobe pituitary gland*. Je, tunaweza kutibu sehemu hiyo ili ikawa hatunusi tena tukishatibu hiyo ikawa inatolewa tu moja kwa moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kujibu katika kifungu (a).

- a. Maradhi mengi yanayotokana na zile *natural gland* ambazo zinaumbwa katika mwili ikiwa ni pamoja na *pituitary gland* hayana tiba. Tiba yake ni mgonjwa kupewa ile *hormone* ambayo amekosa na hususan hii *pituitary gland* ambayo ipo kwenye sehemu ya *posterior lobe* ya ubongo basi nayo haina tiba bali mgonjwa anaongezewa.
- b. Lakini la pili, hizi *glands* zina kawaida ya uwamuzi wake wenyewe, haziamuliwi na *chemical contents* za mwilini, yaani huwa zina uwamuzi wake mwenyewe. Unaweza kukuta kama *pituitary gland* inaweza kukaa muda mrefu haijatoa *hormone* hii ya *anti-diuretic*, lakini ghafla ikaanza. Hata wagonjwa wa sukari hii ya *diabetic mellitus* unaweza kukuta muda mrefu wameekaa wameathirika, *pancreas* yao haijatoa *insulin*.

Lakini kuna *natural process* ghafla *insulin* ile ikaanza kutoa ile *hormone*, uwamuzi wake ni wenyewe. Watu wa dini wanasesma ni *qudra* ya Mwenyezi Mungu, lakini wanasyansi bado wanaendelea kufanya *research* kwamba hizi *hormones* kuwa kitu gani kinasababisha ile *hormone* kutoka ndani ya hizo *gland*. Kwa hiyo, ni *natural process* ya *body* na *communication* au *bio-chemical* ya *communication* ya mwili wa binaadamu.

Mhe. Naibu Spika, anapokosa mgonjwa hii *hormone* ya *anti-diuretic* ndiyo hili tatizo linakuja na ndio maana napewa kitu kama vile vicksi za zamani *anti-diuretic* ambayo inakuwa inanuswa ndani ya puwa ambayo inasababisha kupata ile *hormone* kupitia kwa njia ya hewa.

Upande wa *diabetise mellitus* kama mnavyojua mgonjwa huyu anapewa *insulin*, lakini kunatokea tatizo wakati *pancreas* imeanza kufanya kazi basi na yule mgonjwa akawa hajajua, yaani haendi kila mara kupata kipimo hospitali cha kujua sukari iko kawaida au sukari ipo juu na *pancreas* yake imefanya kazi.

Mhe. Spika, basi kama ulivyo sema kuna *highper stage*, mgonjwa huingia katika kupungua sukari ghafla kwa sababu kuna *insulin* alipiga na ile *pancreas* yake imeshaanza kufanya kazi, sukari hushuka ghafla nayo pia husababisha tatizo mgonjwa anaweza kwenda kwenye *comma* au akaanguka au akapoteza hata fahamu na hisia nyengine za mwili.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mwakilishi, kwamba hili la mwanzo aliloliuliza huwa halina tiba ya moja kwa moja. Tiba yake ni kupata *hormone* na kwa kuwa wagonjwa wake si wengi na kozi yake kubwa ni urithi wa kuzaliwa, hii *insipidus* ni urithi.

Mhe. Naibu Spika, *mellitus* ni mfumo wa maisha pamoja na wengine ambao wanarithi ambao wamepata kutoka kwa wazazi wao. Lakini na mfumo wetu wa maisha unachangia sana kwenye *mellitus*, kwa sababu mtu anapiga sahani ya biriani ile nzima au simia peke yake, sasa ile *pancreas* inatoa idadi maalum ya *insulin*. Kwa hiyo, ile *insulin* inakuwa inazidiwa, chakula kinakuwa kingi, unakula na vyakula vyenyewe ndio hivi vyetu; pilau, biriani na kadhalika na

ile *insulin* inatolewa kwa *quantity* maalum. Kwa hiyo, ile *insulin* inazidiwa ile sukari moja kwa moja ikishavunjwa inakwenda kwenye damu hapo unapata *diabetic mellitus*.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo, hayo ndio majibu ya kutibu hizo *diabetic* za aina mbili, kwa kweli ile *pituitary gland* haina matibabu ya moja kwa moja mpaka kuongezewa kwa hii *hormone*. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika,

- a. Watu wanapopata matatizo ya maradhi haya ya kisukari tunavyoambiwa kuwa dawa yao ni kupata sindano ya *insulin* pamoja na kutumia chakula maalum tunasema *proper diet*. Kwa sababu kuna chakula cha msingi *primary food surface*; moja katika hiyo ni uwanga na binaadamu anatakiwa atumie kwa asilimia 80 katika chakula chake. Kwa vile mtu anapopata maradhi haya anazuiliwa kula aina ya chakula chochote chenye sukari na kukosa sukari katika kiwili wili ni athari kubwa sana, mwili haufanyi kazi ipasavyo, akili inadumaa na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Suala ni kuwa kwa sababu tatizo kubwa ni *insulin*, hakuna utaalamu wa kutosha ili binaadamu asiwe na matatizo haya ili aweze kuendesha maisha yake ya kikawaida hiyo ni moja.
- b. Halafu la pili, kuna baadhi ya madaktari tu kuwa unaweza ukatumia soda kama pepsi dayati kama *Coca-Cola zero* na kadhalika. Zote ukiziangalia zina sukari. Je, kutumia soda hizi kweli ni sawa kwa mtu mwenye matatizo ya sukari au si sawa.
- c. Watu wa aina mbili wanakuwa na sukari ya aina moja, lakini mmoja akipata kijeraha kinakuwa endelevu, lakini mwengine inakuwa kama kawaida, ni sababu zipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, suali la tatu mwisho sikulipata kabisa, naomba kidogo alitolee ufanuzi.

Mhe. Naibu Spika: Rejea la mwisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Na sauti kidogo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Naam!

Mhe. Naibu Spika: Kijeraha

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Swali la mwisho Mheshimiwa ni kuwa watu wanaokuwa na maradhi haya ya kisukari yaani *diabetic mellitus*, sio *insipidus* mara nyingi wanaopata vijaraha huwa ni endelevu au vidonda vinyavyosababisha hata sehemu zake za viungo kukatwa kwa kunusuru isiendelee sehemu nyengine, lakini kuwa wengine haya hayatokei. Je, ni kitu gani kinachosababisha hawa wakipata vijaraha au madonda yanakuwa endelevu na wengine ikawa hali ni ya kawaida.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nitaanza na majibu ya jumla kwanza, wakati tunalipitia suala hili ninazungumza na wataalamu wa Wizara ya Afya tulijaribu kuliangalia kwenda kwenye chanzo, hiyo isitoshe kwenye *research* ya *internet* wanasema wagonjwa wengi walikuwa nchi zilizoendelea wanapopata maradhi haya basi wao wanaishi na maradhi kama haya ni maradhi ya kawaida yaani *natural disease* bila ya kupata vifo na kadhalika. Na wanasema njia kubwa kabisa ni yule mgonjwa kuusoma mwili wake mwenyewe. Kuangalia ile program yake ya mwili wake mwenyewe, kwa hivyo inachukua muda hiyo. Sasa nitatoa mfano mdogo kwa mgonjwa wa maradhi ya kisukari vipi kuusoma mwili wake, kama unatumia *insulin* unatakiwa uusome mwili wako ile *insulin* unatumia kabla ya kula au baada ya kula. Je, dakika ngapi kabla ya kula unatumia sindano ile ya *insulin*. Kuna wagonjwa humu hutumia *insulin* dakika kumi kabla ya kula lakini kwa kuwa mwili wake unapokea haraka sana *insulin* ndani ya dakika tano anaweza kuanguka kama hajapata chakula.

Kwa sababu ile sukari iliyokuwamo ndani ya mwili hushuka ghafila na hushuka kwa haraka zaidi akakosa nguvu kabisa, au akaingia katika *stage* hata ya *coma*. Kwa hivyo muhimu kabisa kwa mgonjwa wa kisukari mbali ya ushauri wa daktari, mbali ya matibabu, mbali ya *insulin* ni kuusoma mwenendo wa mwili wako mwenyewe na kila mgonjwa wa kisukari ana mwenendo wake. Kwa mfano, kuepuka kukata kucha kwenye sehemu kama vile kona hizi, kwa sababu ukipata kidonda kidogo tu umekata hii kucha upande au mdudu upande huku basi inaweza kusababisha kidole chake kizima kikakatwa. Kwa sababu unakuwa na *content* ya sukari kubwa zaidi kwenye damu ambayo huchukua muda kwa kidonda kile kupona. Na mara nyingi sukari ndio inawaalika viumbe hawa wengine *micro organism* ili kuota. Hata kule *laboratory* wanapofanya *test* huwa wanatia sukari wale wadudu kuota, kwa hivyo nayo inavutia. Kwa hivyo ukishapata kidonda damu yako ina sukari na hawa wadudu walioko kwenye hewa ya kawaida basi na wao husababisha matatizo. Hilo ni moja.

Lakini pili, Mhe. Naibu Spika, mara nyingi wanasema hii sukari hupiga maeneo ambayo yapo *extra sensitive* yaani *nerve* zilipokuwepo nyingi, mfano macho kuna *nerve* nyingi sana ambazo zinazosaidia kupata kuona. Kwa hivyo kuna sukari ambayo inamuathiri mgonjwa kwenye macho kwenye viungo vyengine vilivyokuwa na *senses* kubwa zaidi. Nadhani siwezi kuvitaja vyote ndani ya Baraza lakini wajumbe watakuwa wamenifahamu viungo vyenye hisia kubwa zaidi huwa vinapigwa na maradhi haya kwa sababu ina-*effect* maeneo hayo.

Lakini wakati huo huo Mhe. Naibu Spika, ni muhimu sana kubadilisha mfumo wa maisha hasa kwa mgonjwa wa sukari wengine huwa wanaita maradhi ya kitajiri. Lakini mimi naita maradhi ya kawaida Mwenyezi Mungu anakujaalia ni kubadilisha mfumo wa maisha. Kula vyakula vyenye *natural content* zaidi, vyakula hivi wanavyosema *ziro coke* au *diet coke* vipo vingi kuna *diabetic chocolate* kuna zile chakleti za sukari, kuna wale wanaojidanganya wengine samahani, huwa anatia vidonge vya *saccharine* lakini anatia vinane kwenye chai yake. Vile vidonge vya *saccharine* unatakiwa utie viwili kwa sababu ile ni *soluble sugar* ambayo inayeyushwa haraka ndani ya mwili. Lakini utamkuta mtu anatia ile ile anataka iwe shira kama ile shira ya sukari ya kawaida basi na vidonge vile anatia vinane. Sasa pale Mheshimiwa hata ile *soluble sugar* inakuwa ni nyingi ndani ya mwili na mwili pia unapata tabu wa kuyayusha haraka. Kwa sababu ni *soluble sugar* lakini wakati huo huo umetia kwa wingi sana ndani ya mwili.

Kwa hivyo hata mtu kama anakunywa hiyo *diet coke* kwa kujiridhisha na kukidhi mahitaji ya roho yake kujiburudisha basi asinywe *diet coke* nane anywe hiyo moja au nusu ikiwezekana. Kwa sababu akinywa hizo kupitiliza kwa kiwango sukari inakuwa ile ile mwilini. Kwa sababu kinachoingia ndani ya mwili kinakuwa na *content* fulani ukiacha maji ya kunywa. Maji ya kunywa ndio wanasema ndio the *healthiest* hayana sukani kabisa *content* ya sukari na hayana *content* ya *fat* lakini vyakula vyote vyengine unakuta vichembe chembe vya *fats* ama *carbohydrate* ama *sugar* inakuwemo humo ndani.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, kuhusu vyakula hivyo nimejibu, mwisho kabisa nilisema pale awali kwa wale wanaopata dawa hii *mellitus*, wanaopata hizi *insulin* mgonjwa anatakiwa yeze mwenyewe asome kama anapata *five zile mills* za *insulin* akiona anaanza kuona kizungu zungu basi yeze mwenyewe anatakiwa ende kwa daktari akapime na kumuuliza daktari jana mimi nilipiga kiasi fulani cha dawa lakini baada ya kupiga kiasi fulani cha sindano au dawa nimeona kizunguzungu je, vipi nipunguze au niongeze dozi na pale kwa vipimo vyengine ndio atakapoweza kushauriwa kama anatakiwa aongeze dozi au apunguze. Kwa hivyo jukumu la kusoma mwili pia ni la mgonjwa hususan wale wanaotumia *insulin* aidha za vidonge kama vile *glibenclamide* na wale wanaotumia sindano.

Naomba nimalizie hapo Mhe. Naibu Spika. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru Mheshimiwa pamoja na majibu lakini umetupa na taaluma. Tunaendelea.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, swali la mwisho sijajibiwa.

Mhe. Naibu Spika: Linahusu nini. Nilisema kuna watu wengine wanapopata madonda au majaraha huwa ni endelevu lakini kuna wengine wana maradhi hayo ya kisukari wakipata vijaraha vinakuwa katika hali ya kawaida. Kwa hivyo nikitaka ufanuzi kupata maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nadhani jibu hili nililitoa labda sijalitolea ufanuzi tu, nilisema hivi kwa wale wagonjwa hasa wenye sukari ya damu na sukari yao iko *uncontrollable* yaani viwango inakuwa mara nyingi kubwa zaidi basi wale wagonjwa wajitahidi sana waepuke na kupata jeraha la aina yoyote, nikatoa na mfano wa kukata kucha. Mfano mdogo tu wa kukata kucha hizi mgonjwa wa sukari kwake yeze kukata kucha ni hatari zaidi kuliko binaadamu wa kawaada aliyezwa hana ugonjwa wa sukari. Kwa hivyo kiwango cha sukari kikiwa kikubwa katika damu na ukapata jeraha basi pale ndipo panapopelekeea lile jeraha kuwa kubwa na kile kidonda kuwa kikubwa na sehemu ile ya jeraha ikaanza kuoza kwa sababu inakuwa haipati *supply* ya kutosha ya damu kwa sababu damu inakuwa nzito kama vile maji ukiyatia sukari ndani inakuwa maji ya shira yale maji yanakuwa mazito, tuchukulie kama shira ya kaimati inakuwa kama vile, kwa hivyo inakuwa nzito zaidi na ile damu inakuwa haifiki eneo lile ndiko kunakopelekeea mgonjwa kukatwa kwa kiungo kile kwa sababu kinaanza kufa kabla ya maeneo mengine.

Mara nyingi inabidi ukate sehemu ile kwa sababu eneo lile likisha kufa husababisha kuoza na ule muozo kuweza kutambaa ukaingia eneo jengine ndio maana inabidi uwahi haraka sana. Wale wagonjwa ambaa naweza kusema sukari yao imo katika mkojo zaidi kuliko kwenye damu au damu inakuwa sukari ndogo wale ni afadhali majeraha yao huwa yanachukua muda mrefu sana kupona. Lakini wanakuwa hawana haja ya kukatwa mara nyingi viungo. Na madaktari wanakwepa sana kukata kiungo, hujaribu kwanza kikitibu kiungo mpaka kipone, pale inaposhindikana kabisa na kiungo kile kikawa tayari kimeshaanza kufa eneo lile madaktari huwa wana hofu kwamba kufa kwa kiungo kile ama eneo lile kukosa maisha kusije kukaambukiza na eneo jengine ndio huwa wanakatwa. Na utakuta wakianza kukata hawaanzu kukata eneo lote wanaanza na kidole halafu anawezakuja na eneo zima la kidole, wengine hukatwa mguu kipande, wengine eneo zima la mguu mpaka tena inapofika hali ya juu kutokana na kutambaa kwa kifo kile cha eneo lile kutokana na sukari kuwa nyingi na damu kutofika eneo lile. Mhe. Spika, ahsante sana.

HOJA YA MJUMBE

Hoja ya Kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa Maazimio Kuhusu Uimarishaji wa Huduma za Afya Zinazotolewa kwa Wananchi wa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ninafarajika kumuona Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi na msaidizi wake Mhe. Mohammed Aboud na kama unavyoona ukumbi ulivyo lakini wahusika wakuu wapo kuhusu suala hili, ninashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nianze maelezo, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dr. Ali Mohammed Shein imekuwa na malengo ya dhati kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wake ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kujenga taifa lao;

Na kwa kuwa katika kuhakikisha kwamba lengo hilo linatia Serikali imekuwa na Sera ya Sheria pamoja na mikakati mizuri ya kuwapatia wananchi huduma bora za afya. Na kwa kuwa Serikali inaelewa kwamba maendeleo ya nchi yoyote yanategemea nguvu kazi ya wananchi wake ambao inapatikana kutoka kwa wananchi wenye afya iliyio imara;

Na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali za kuimarisha huduma hizo mijini na vijijini ikiwa na pamoja kujenga vituo vya afya katika maeneo mbali mbali ili kuziweka karibu na huduma za afya kwa wananchi lakini pia jitihada za kununua vifaa vya matibabu ili kukabiliana na magonjwa mbali mbali yanayoendelea kuzuka katika jamii yetu siku hadi siku;

Na kwa kuwa katika kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa watu wenye utaalamu wa hali ya juu, Serikali husomesha wataalamu nje ya nchi lakini pia imeanzisha Chuo cha Elimu ya Sayansi ya Afya kilichopo Mbweni ili kuweza kuwasomesha wananchi wa Zanzibar katika fani mbali mbali zinazohusu masuala ya afya, ili hatimaye wataalam hawa waweze kutumika katika hospitali na Vituo vya Afya viliopo chini kwa lengo la kutoa huduma kwa wananchi;

Na kwa kuwa sisi viongozi wa wawananchi tunashuhudia kuziona jitihada hizo ambazo zina azma ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na hivyo kupaswa kuziunga mkono. Jambo la kupongezwa Mhe. Naibu Spika.

Na kwa kuwa pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa katika hospitali zetu ni nzuri bado kuna changamoto kubwa katika kufikia azma hiyo kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu, ukuaji wa teknolojia na kasi ya kuibuka kwa magonjwa mapya;

Na kwa kuwa tegemeo kubwa la wananchi wa Zanzibar ambao hawana uwezo wa kupata matibabu nje ya nchi lipi kwa hospitali kuu ya Mnazimmoja ambayo Serikali ina lengo la kulifanya hospitali ya Rufaa na hospitali nyengine za Serikali pamoja na vituo vya Afya, sisi wawakilishi wa wananchi hatuna budi kuikumbusha Serikali kwamba kuna kazi kubwa ya kuimarisha hospitali hiyo kwa Zanzibar na hospitali nyengine ndogo ndogo. Hivyo basi jitihada za makusudi na za haraka ni lazima zichukuliwe ili kukuza kiwango cha huduma kinachotolewa katika hospitali hiyo pamoja na kuziimarisha hospitali nyengine ndogo ili ziweze kutoa huduma za awali kabla tatizo halijapelekwa katika hospitali ya rufaa.

Na kwa kuwa hali ilivyo sasa hospitali hiyo ya Mnazi Mmoja na nyengine nchini zinakabiliwa na uhaba wa wataalam wa afya katika fani mbali mbali ambao wanahitajika kutoa huduma za maradhi makubwa ambayo yanaonekana kukabiliwa na wananchi wengi wa Zanzibar;

Na kwa kuwa takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kwamba hali ya upungufu huo wa wataalamu ni kubwa sana kwa mfano, takwimu zilizotolewa na Mhe. Waziri wa Afya wakati akisoma hotuba ya bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2012/2013 katika kiambatanisho namba 10 zilionesha hali halisi ya mahitaji ya wafanyakazi katika hospitali ya Mnazimmoja ambapo kwa jumla zilionesha kwamba mahitaji makubwa sana kuliko kiwango kilichopo sasa. Kielezo hicho kinaambatanishwa pamoja na maelezo haya.

Mhe. Naibu Spika, si vibaya kwa faida ya wananchi tukakiangalia mwisho kiambatanisho namba 10 hiki tukaiona hali ilivyo.

Kada	Mahitaji	Waliopo	Upungufu
<i>General Physician</i>	1	0	1
<i>Cardiology</i>	3	1	2
<i>Pharmacist</i>	4	1	3
<i>Nephrology</i>	4	0	4
<i>Radiologist</i>	6	1	5
<i>Haematology</i>	6	1	6
<i>Anaesthesiology</i>	8	1	7
<i>Dermatology</i>	8	0	8
<i>Oncology</i>	9	0	9
<i>Psychitry</i>	10	0	10 hatujapiga hatua bado hapo.
<i>Surgeon</i>	12	1	11
<i>Obstetrics and gynaecology</i>	14	2	12 bado kazi ipo.
<i>Paediatrician</i>	14	2	13
<i>Dentist Specialist</i>	15	2	13
<i>Medical Officer</i>	24	14	14 sio mbaya sana.
<i>AMO (Assistant Medical Officer)</i>	28	14	14
<i>General Nursing</i>	234	218	16
<i>Anaesthetic Nurse</i>	24	7	17
<i>Paediatric Nurse</i>	18	0	
<i>Psychitric</i>	60	41	19 sio mbaya sana.
<i>Dental Nurse</i>	20	0	20 bado pana kazi.
<i>Laboratory Technician</i>	59	38	21
<i>Ophthalmic Nurse</i>	25	3	22
<i>ENT Nurse</i>	23		0 hapajafanywa jambo bado.
		24	

<i>ICU Nurse</i>	24	0 tupo pale pale bei ya pilipili hoho.
<i>Orthopaedic Nurse</i>	26	26 bado hii hali nzito.

Mhe. Naibu Spika, niendelee. Mwaka 2009/2010 jumla za dola za Kimarekani 369,238 zimetumika kuwatibu watu 73 nje ya nchi. Hizi ukizi-change kwa *rate* ya leo karibu milioni mia sita au ishirini na saba. Mwaka 2010/2011 jumla ya shilingi 906,295,038 zimetumika kuwatibu wananchi zaidi ya 60 nje ya nchi.

Mwaka 2011/2012 jumla ya shilingi 616,091,417 zimetumika kuwatibu wananchi 157 nje ya nchi. Mwaka 2012/2013 jumla ya shilingi 990,248,168 zimetumika kuwatibu wananchi 144 nje ya nchi.

Mwaka 2013/2014 jumla ya shilingi 2,5,97,115,697 zimetumika kuwatibu wananchi nje ya Zanzibar. Na kuna wengine pengine hawajapata bahati hii kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kuwaponesha.

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa uchunguzi huo inaonekana dhahiri kwamba fedha nyingi zinatumika kwa matibabu nje ya nchi mbali na gharama nyengine zinazotumika, kuwatibu wananchi Tanzania Bara, ambapo fedha hizi zingeweza kutumika kuimariswa hospitali zetu kuwapeleka wataalamu kusomea ujuzi wa kutibu maradhi yanayoshindikana hapa nchini kwa sasa na ununuzi wa vifaa vyta kisasa vyta uchunguzi na matibabu, ambapo hatua hiyo ingeweza kuipatia nchi madaktari bingwa wengi, kwa muda mfupi zaidi na hatimaye wananchi wangeweza kupata matibabu hayo hapa nchini.

Na kwa kuwa, bado wagonjwa wanaokosa nafasi ya kutiba nje ni wengi kutokana na ukosefu wa fedha kama ilivyoletwa na Mhe. Waziri wakati akisoma Hotua ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 ambapo alisema:

"Mhe. Spika, licha ya kuimari baadhi ya huduma katika Hospitali zetu, bado wagonjwa wanaoshindikana nchini ni wengi. Hali ya uchumi wa nchi yetu umefanya wagonjwa wengi kukwama wengine kupoteza maisha, wakati inasomwa hotuba hii kuna wagonjwa wasiopungua 190 amba wanasubiri fedha kupelekwa matibabuni nje ya nchi". Ukurasa wa 43.

Mhe. Naibu Spika, hayo sio maneno yangu, hayo ni maneno ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa hali hiyo inaonesha kwamba bado mazingira yanaonesha kupatikana kwa matibabu bora ndani na nje ya nchi hayajafikia kiwango kinachotakiwa kutokana na ubaha wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya hospitali zinazotakiwa kutokana na huduma hizo. Kwa mfano, Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo ndiyo Hospitali Kuu kwa Zanzibar. Takwimu za miaka mitatu iliyopita zinaonesha kwamba fedha zilizotengwa na zinazopatikana kwa ajili ya Hospitali hii ni kidogo sana kuweza kutosheleza mahitaji yake kama inavyoonekana hapa chini.

Mwaka wa fedha 2011/2012, fedha zilizotengwa shilingi 262,178,000, fedha iliyopatikana kwa mwaka 197,839,070 ni sawa na asilimia 75. Mwaka 2012/2013 fedha zilizopatikana shilingi 642,000,000, fedha iliyopatikana 410,785,579 sawa sawa na asilimia 63. Mwaka 2013/2014, fedha zilizotengwa shilingi 1,291,199; fedha iliyopatikana kwa mwaka 666,675,500 sawa na asilimia 54. Kila tunapokwenda tunazidi kushuka, badala ya kuongeza bado tunateremka ni kitu cha kusikitisha sana hiki.

Hivyo, kwa tathmini hizi inaonesha kwamba kuna haja ya serikali kuweka kipaumbele cha huduma za avya kwa kuongeza kiwango cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya huduma hii ikiwemo vifaa, kusomesha wataalamu na kununua madawa na kadhalika.

Na kwa kuwa inaonekana kwamba, Serikali inaongeza jitihada ya kusomesha wataalamu wa afya katika fani mbali ili kuzipa uwezo hospitali zetu kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kwamba idadi ya wataalamu wanaopelekwa kusoma ni ndogo na hawajielekezi katika kusomea fani ambazo zina upungufu wa wataalamu nchini.

Kwa mfano, takwimu za wanafunzi walokwenda masomoni kwa mwaka 2013/2014 zinaonesha kwamba jumla yao ni 142, kati ya hao 78 wamesomea *nursing*, 13 *medical laboratory*, 12 *AMO (Assistance Medical Officer)*, 11 ni *BMS* nafikiri itakuwa ni *degree* ya kwanza hii ya daktari, wataalamu sijui wanasema ni *Bachelor of Medicine and Surgery* kitu kama hivyo. Wataalamu katika fani zinazohusiana na magonjwa sugu yanayokabiliwa na wananchi ni mfano au tathmini za mwaka huo zinaonesha kwamba maeneo muhimu kama *enology* yanahuusu magonjwa ya

Sukari, au *Orthopedic Surgery* yanaohusu tiba ya magonjwa waliovunjika viungo, *oncology* yanahusu matibabu ya kensa, *pediatrician* yanahusu tiba za watoto wadogo, *internal medicine* yanahusu tiba ya maradhi ya moyo, mapafu na kadhalika na maeneo mengine ya wataalamu waliokwenda masomoni ni mmoja tu katika kila fani.

Takwimu hizi kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015 ukurasa wa 83. Si kazi rahisi kutafuta vitu kama hivi, ilikuwa kazi kidogo kupata *data* na kwa kuwa takwimu za wataalamu wanaorudi masomoni wengi ni wa ngazi ya chini kuliko ngazi ya juu, hali iliyopelekeea kukosa wataalamu mabingwa kutibu maradhi mbali mbali. Kwa mfano, takwimu za wanafunzi waliorudi masomoni mwaka 2012/2013 ni wengi kati ya ngazi ya cheti 14 na ngazi ya *degree* ya kwanza 34, kati ya hao ni 16 wanaosomea *nursing*. Katika ngazi ya *post graduate* ni mmoja tu, ngazi ya *master* ni wanne na ngazi ya *PhD* ni mmoja. Takwimu hizi kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya ya mwaka 2013/2014, ukurasa wa 101.

Mhe. Naibu Spika, hii ni dhahiri kwamba bado kuna kazi kubwa ya kujielekeza katika kuwekeza katika kusomesha wataalamu wengi ili kuweza kuepuka matumizi ya gharama kubwa za kuwatibu wananchi nje ya nchi. Lakini pia kuwapatia wananchi huduma bora zaidi za afya na kwa kuwa bila kuhakikisha kwamba hatua za haraka haraka zimechukuliwa na serikali, ili kuweza kuondoa mapungufu hayo kuhakikisha kwamba huduma za kuelimisha zinapatikana katika hospitali zetu. Kwa kuwa sisi Wawakilishi wa wananchi tuna jukumu la kusimamia serikali katika kuhakikisha kwamba majukumu yake yanatekelezwa katika kiwango cha kuridhisha, kwa kuishauri serikali katika mambo mbali mbali yanayohusu maslahi ya wananchi ikiwemo suala hili muhimu.

Kwa hivyo basi, mimi Jaku Hashim Ayoub, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kuititia Jimbo la Muyuni chini ya Kanuni ya 27(1)(m), 27(3), 49(1) na 50 za Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2012, naliomba Baraza lako lipitishe maazimio yafuatayo:

(1) Kwamba serikali ifanye mabadiliko ya kisera yatakayoiwezesha serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu wetu nje ya nchi, ili waweze kuwashudumia wananchi baada ya kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka wagonjwa nje ya Zanzibar.

(2) Kwamba mabadiliko hayo ya kisera yaende sambamba na kuwa na mkakati wa kusomesha kwa awamu wataalamu wa fani ambazo zina upungufu, hususan katika magonjwa sugu yanayoshindikana kutibiwa ndani ya Zanzibar na kuacha kujikita katika kusomesha wataalamu katika fani hizo, kwa hizo ambazo tayari zina wataalamu wa kutosha.

(3) Kwamba serikali ifanye mabadiliko ya kimfumo kwa bajeti kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 utakaowezesha kupunguza kwa kiwango maalum bajeti zinazotengwa katika sekta nyengine ili kuweza kuongeza kiwango cha bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya nchini itakayowezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa matibabu pamoja na kusomesha wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali.

(4) Kwa kuwa serikali kuititia Wizara ya Fedha ijihakikishe kwamba fedha zinazotengwa katika bajeti ya serikali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya zinaingizwa zote kwa wakati, ili Wizara ya Afya iweze kutimiza wajibu wake na mipango.

Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Fedha hatujamuona kipindi kirefu hapa hili lilikuwa linamuhusu ye ye zaidi.

(5) Kwamba serikali ifanye mabadiliko ya mishahara ya maslahi ya wataalamu wa afya ili kuwapa moyo wataalamu wetu na hivyo waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, lakini pia kwa kuwa maslahi mazuri yatakayopelekeea wataalamu hao kubaki nchini na kuhudumia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitilie mkazo tena kwa kurudia tena kifungu hiki muhimu namba 5 ambacho wataalamu wengi huwa wanakililia hivi sasa. Namba 5 ni kwamba serikali ifanye mabadiliko ya mishahara na maslahi ya wataalamu wa afya ili kuwapa moyo wataalamu wetu na hivyo waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Lakini pia kwa maslahi mazuri yatakayopelekeea wataalamu hao kubaki nchini kwa kuwashudumia wananchi.

(6) Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Bodi ya Mikopo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wajielekeze katika mpango wa muda mrefu wa kusomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini.

(7) Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kwamba serikali iandae mikakati madhubuti na yenye kutekeleza ndani ya muda mfupi kwa ajili ya kujaribu kuwarejesha nchini wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali waliokimbia sehemu mbali mbali za duniani kwa sababu mbali mbali ikiwemo maslahi.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wetu wengi hivi sasa wanakimbilia Tanzania Bara kutokana na maslahi ya hali ilivyo; ni kwamba nitoe ushauri serikali ilifikirie suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Waheshimiwa hoja imetolewa na mwenzetu Mhe. Jaku Hashim na mpaka hivi sasa nimepata jina moja tu la anayetaka kuchangia hoja hii na wa pili Mhe. Saleh Nassor Juma. Kwa hivyo, namuanza Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii, hatunabudi sote tumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kutupa pumzi kufika katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, pili napenda kumpongeza kwa dhati kabisa ndugu yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa hoja yake hii aliyoitoa ambayo nasema hoja hii aliyoleta imejaa hekima, busara na usikivu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kiti nilichokalia mimi humu, mimi nimekuja kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi nikiwa kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na ndivyo nilivyo hapa mbele ya kiti hiki, sikuja tu humu ndani katika Baraza la Wawakilishi isipokuwa nimekuja kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim kaelezea mengi na hii ni changamoto yetu sisi sote Wazanzibari. Kama unavyoelewa serikali yetu imefanya mambo mengi sana katika barabara, afya, umeme, huduma nyingi sana. Lakini vile vile na uchumi wetu sasa kila tukienda unazidi kuwa wa kimasikini. Sasa hapa tunasema *we have a problem* na tunataka kukaa sisi tunasema lazima tutafute *solution*, halafu tunasema *what is next*.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiri tukubali sote kuwa Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo ndiyo inayotekelza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, changamoto ziko nyingi sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Jaku na mambo mengine sana, lakini nafikiri tukubaliane kwamba hili ni letu na tunatakiwa sisi mwanzo kama Zanzibar au Wazanzibari tuijulize tumeichangia nini Wizara hii ya Afya au tumeichangia nini Zanzibar.

Zanzibar ina historia ndefu katika mambo haya na kama tutakaa pamoja na wizara inayohusika na serikali yetu changamoto hizi zilizokuwewko zinaweza zikapungua kwa kila sehemu. Lakini vile vile tatizo kubwa ninaloliona mimi sio kila anayepepesuka ni mlevi, tatizo kubwa ninaloliona mimi ni urasimu au ni utendaji tu wakati mwengine katika kukabidhiana mambo yetu haya.

Kwa mfano, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Uzini natoa mfano. Serikali ishafanya mengi sasa sisi kama Wawakilishi, Wabunge, Wafanyabiashara na Wafadhili tunatakiwa kuchangia maeneo mbali mbali, kwa sababu huu ndio utamaduni wetu.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana mimi nilipata shilingi milioni kumi na tano kwa ajili ya wananchi katika jimbo langu, tukakubaliana na wananchi wa Uzini pesa hizi ambazo zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa tukakubaliana kunununa dawa. Kwa hivyo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikaniingizia shilingi 15 milioni katika jimbo langu la Uzini. Lakini naweza kusema ni mambo mengi tu, nikaandikia Wizara ya Afya barua mwaka jana na mwaka huu kuwaambia kwamba ninazo shilingi 15 milioni kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini, naomba pesa hizi tutumie katika kuiunga mkono Wizara ya Afya, kuiunga mkono

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kununulia madawa, kwa kuongezea madawa kwa ajili ya Jimbo la Uzini.

Mhe. Naibu Spika, sasa changamoto iliyokuweko kwa kweli nilikuwa nafuutilia mwenyewe. Kwa bahati nzuri tarehe 26 mwezi huu wa Septemba ndipo nilipopewa rasmi barua ya Wizara ya Afya na *list* ya madawa ya hizi shilingi 15 milioni. Sasa kilichokuwepo naweza kusema ni changamoto au vile vile uzito wa jambo na wakati hii ilikuwa ni msaada kuisaidia Wizara ya Afya Jimbo la Uzini. Sasa zile pesa ndiyo nimeanza kufuutilia wameniandikia orodha, tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeniandikia barua kuna shilingi 20 milioni nyengine za wananchi wa Jimbo la Uzini. Sasa napata tabu kwa sababu zile sijazitumia na hizi siwezi kuzipokea. Mhe. Naibu Spika, mimi ningeliomba Wizara ya Afya kwamba tukaeni kwa pamoja kuona jinsi gani tunawenza kuchangia.

Lakini vile vile kuna wafadhili. Juzi nilikuwa na Dokta Azaan Bin Braik huyu ni Daktari Bingwa wa *Heart Duniani yuko Dubai pale*, nilikuwa nimezungumza naye na akaniambia kwa nini Mheshimiwa Mohamedraza tusiletu timu ya madaktari Zanzibar au sehemu yoyote kwa gharama zao ili kuja kuwasaidia ndugu zetu Wazanzibari katika suala la ugonjwa wa moyo ambalo ndio changamoto kubwa.

Vile vile kuna vitu hivi lazima wizara inayohusika ivifanyie kazi. Kwa mfano, juzi mwezi uliopita Makamu wa Kwanza wa Rais Al-Hajj Dr. Mohammed Gharib Bilal amekwenda kufungua Kituo cha Afya Ndaga Jimbo la Uzini. Mimi kama Mwakilishi katika kupewa changamoto sina taarifa lakini nilipopeleka barua Wizara ya Afya kuwaambia kwamba bwana mimi ni mdau wenu, mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini amekwenda Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mzee wangu Dokta Bilal. Wizara ya Afya imenijibu kwamba wala wao hawakuwa na taarifa na wao wamealikwa tu, yaani Wizara ya Afya na wao wamealikwa amekwenda kiongozi, kwa bahati nimekwenda Ndaga, kile kituo kina mapungufu hakuna daktari sasa, amepelekwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Afya na wao wamealikwa kama washiriki.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi ningeliomba Wizara ya Afya au Serikali kwa sababu unapofanya Kituo cha Afya kama Wizara ya Afya hawajajiandaa na madaktari, hawajajiandaa na mambo ambayo wana changamoto zao nyingi tunawenza kupata tabu sana katika kuendesha wizara hii na wizara hii ni kubwa sana. Bajeti waliyokuwanayo haiwezi kukidhi Wazanzibari na Watanzania kwa jumla kutokana na hali ya uchumi ilivyo, hasa na bajeti hii waliyoandikiwa. Inaweza ikawa serikali yetu vile vile kutokana na mazingira ya uchumi isitimize bajeti hii katika kusaidia. Sasa mimi naomba nitoe changamoto kwa serikali na mimi niko tayari kuitumikia serikali kwamba serikali iunde kamati maalum ambayo itaweza kusaidia upatikanaji wa dawa na utaalamu na kuwasaidia madaktari na kusaidia serikali yetu hasa katika Wizara ya Afya ambayo kamati hiyo kati yake itakuwa kuhamasisha Wazanzibari walioko nje na ndani ya Zanzibar, ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania katika kusaidia sehemu nyingi sana katika Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, utumishi huu mimi nautaka sitaki posho, sitaki mshahara wala sitaki nauli ya kusafiri kwa sababu Mwenyezi Mungu amenijalia nimefika kwa niaba ya wananchi na wananchi ndio walioniwezesha mimi nikafika hapa. Lakini vile vile nimesomeshwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika elimu yangu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeliomba kwamba sehemu nyingi Serikali ingelikaa sasa kutafuta, Wazanzibari wapo Mheshimiwa haya madawa, vyakula ni mambo madogo sana. Mhe. Naibu Spika, huko nje kuna Wazanzibari wenye uwezo mkubwa sana wa kusaidia mambo kama haya, lakini yanataka ufatiliaji, yanataka uwe mzungumzaji, yanataka uwe umechoka kuelezea shida yako.

Mhe. Naibu Spika, huwezi kukaa kwenye kiti ukakizungusha tu hichi ni vigumu sana. Kwa hivyo, kama tumekuwa watumishi humu ndani sote tumekuja kwa niaba ya watumishi wa kila mtu jimbo lake. Mimi hapa ni mfanyakazi wa jimbo la Uzini ni mtumishi wa Jimbo la Uzini kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, tuna uchungu na nchi yetu, kwa hivyo mimi nafikiri hoja aliyoizungumza Mhe. Jaku Hasssan imefika wakati sasa changamoto iliyokuweko tupewe orodha tu ya madawa, hapa iletwe orodha tu madawa haya

yanapatikana sehemu fulani. Mhe. Naibu Spika, tunaweza kusaidia, tunaweza kuwapunguzia maisha magumu. Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengi.

Mhe. Naibu Spika, suala la Afya kwa Unguja na Pemba tunaweza kupata vituo vya kutosha, tunaweza kupata madaktari wa kutosha tukijipanga. Kwani Mhe. Naibu Spika, hata hizi sherehe zetu tunazozifanya kila mwaka au mambo mbali mbali ni kujipanga. Sasa tukijipanga mimi nafikiri tutaipunguzia serikali mzigo huu. Mimi wito wangu Mhe. Naibu Spika, ningeliomba kwamba kutokana na hali ya afya kwa kweli wananchi wengi waliokuwa hali zao za chini ndio wanaoumia sana. Sisi mara nyngi kutokana na uwezo, kutokana na umaarufu wengi tunatibiwa nije.

Kwa hivyo, imefika wakati Mhe. Naibu Spika, kuiomba Wizara ya Afya ikae itafute njia waseme wanahitajia mfano watafute viwanja visiwa vya Unguja na Pemba waseme bwana tunahitajia Vituo vya afya, waseme kwamba wanahitajia mashine ya aina hiyo, wanahitajia madawa ya aina hiyo na waseme madawa haya yapatikane kutokana na nchi fulani.

Sasa Mhe. Naibu Spika, yataondoka na mambo mengi sana hata Hospitali ya Mmazi mmoja hata kukiwa na upungufu wa chakula Mnazi mmoja. Mhe. Naibu Spika, ndio hali yetu hai hoi. Mimi sidhani kama Serikali yetu inapenda kuona wananchi wake wanaumia katika masuala ya kiumasikini. Lakini tunapotaka kuondosha umasikini lazima tuwe *serious* katika uondoshaji wa umasikini.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, Mnazi mmoja hapa kuna changamoto nyngi sana kuna wengine pale hali zao hai hoi wanawenza kutoka shamba pale nauli hawana wakafika pale daktari asipatikane, Mheshimiwa vitu hivi lazima uvitizame na hii inasaidia sana Mhe. Naibu Spika, kwa madaktari wetu na wauguzi wetu tuwawezeshe katika posho zao na hivi vinaweza vikafanyika.

Mhe. Naibu Spika, kama Bajeti ya Wizara ya Afya wanasema chakula chao milioni kumi kwa mfano kwa mwezi. Hebu wajaribu kuniletea mimi tu orodha ya mikate mingapi, mchele gunia ngapi na mafuta mageloni mangapi basi Mheshimiwa mimi naweza hata miezi miwili tu toka sasa hivi kila mfanyakishara Mzanzibari akachukuwa yaani posho ya mwezi mmoja mmoja utakuta mwaka mzima pale patakuwa na hali nzuri ya afya.

Lakini Mhe. Naibu Spika, unaposema kwamba bajeti ipo panahitajika madawa lakini hali yetu ya fedha Wizara ya Fedha ni ngumu kwa siku zile pesa haipo sasa maana yake kama pesa haikuingia ina maana yule mgonjwa hawezi kutibika kwa sababu mkate hakuna. Sasa hili Mhe. Naibu Spika, lazima tulitizame Serikali yetu itatoa pesa kutokana na makusanyo ya wafanyakishara na wananchi. Sasa makusanyo kama yamekuwa madogo hiyo Wizara ya Afya pesa wanazozipata kwa mwezi ni milioni kumi na makusanyo yakiwa madogo *automatically* Mhe. Naibu Spika wizara ile inapata milioni mbili kati ya milioni kumi ina maana tayari pale mapungufu yaliokuwa yamekusudiwa yatakuwa hayapo na kama hayapo wale waathirika ni wananchi waliokuwa masikini.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ili kuondosha haya tutake Wizara hii ya Afya itoe orodha mimi niko tayari kutembea Tanzania nzima pamoja na wenzangu kuona kwamba tunasaidia nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, nishukuru sana kwa muda huu ulionipa lakini nataka sio wizara hii ni wizara zote Miundombinu, Wizara ya Maji na mambo mengine. Leo pale Waziri wa Maji yupo hapa kuna *pump* ghafla imeharibika Mhe. Naibu Spika, samahani kwa kuanzia tu kuanzia *pump* hiyo haiko kwenye Bajeti sasa utakwenda kumuumiza bure waziri maana yake haiko kwenye bajeti *pump* hii. Lakini sisi kama Wazanzibari wafadhili kwa sababu suala la maji ni muhimu vile vile tukaeni pamoja kuona jinsi gani tunaweza kujengwa Zanzibar na tunaweza kuona kwamba tunashirikiana pamoja.

Mhe. Naibu Spika, na mwisho nawaomba wenzangu kwa heshima zote na taadhima tubadilikeni tujenge Zanzibar. Ahsante sana (*Makofii*).

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya hoja ambayo mwenzetu Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameweza kuiwasilisha hapa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nichukuwe fursa hii kumshukuru sana ndugu yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kukaa na kuwazia kuleta hoja hii ambayo ni ya msingi nzito na yenye kuleta kila aina ya kuona kwamba Mhe. Jaku kwa kweli yuko makini sana katika kuhakikisha kwamba afya za kila Mzanzibari zinaendelezwa na zinakuwa nzuri

sana katika nchi yetu kwa lengo na madhumuni ya kuendeleza taifa letu hali ya kwamba watu wake wakiwa wako wazima sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo sasa mimi naomba kujikita katika maeneo mawili matatu katika hoja hii ambayo ndugu yetu ameileta. Eneo la kwanza ni katika ukurasa wa tano ambapo mwenzetu Mhe. Jaku Hashim alikuja na takwimu hapa. Mhe. Jaku Hashim ametupa takwim za uingizwaji wa fedha katika Wizara ya Afya kwa mwaka 2011/12, 2012/13, 2013/14, na akamaliza kwa 2014/15.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia takwim hizi ambazo zimeelekezwa hapa inaonekana kwamba pamoja na mahitaji muhimu na uzito wa Wizara hii ya Afya ndani ya visiwa vyetu nya Zanzibar lakini kumekuwa na utaratibu wa kuteremka kwa asilimia 10 mpaka 15 kwa kila mwaka. Sasa ukiangalia umuhimu ambao upo katika wizara hii na namna ambavyo takwim za mapato yao zinashuka kwa asilimia kumi na kidogo kwa kila mwaka.

Hii nahisi labda huenda ikawa ni hoja kati ya changamoto ambayo imemsababisha Mhe. Jaku Hashim aweze kutengeneza kitu kama hichi na aweze kutuwakilishia hapa kwa lengo la kutunabahisha kwamba pamoja na hali yetu tuliyonayo kifedha. Lakini bado kuna mambo ya msingi ambayo Serikali yetu kuu inapaswa kuyaangalia, kuyafatilia na kuhakikisha kwamba kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa nakwenda katika ukurasa wa 6. Ukurasa wa 6 Mhe. Naibu Spika, unaelekezea kifungu kidogo cha pili kutokea juu kule naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika:-

"Na kwa kuwa takwimu za wataalamu wanaorudi masomoni wengi ni wa ngazi ya chini kuliko ngazi ya juu hali inayopelekea kukosa wataalamu mabingwa wa kutibu maradhi mbalimbali".

Kwa mfano takwimu za wanafunzi wanaorudi masomoni mwaka 2012/13 wengi ni katika ngazi ya Cheti yaani 14 na ngazi ya Digrii ya kwanza ni 38 kati ya hao 16 wamesomea *nursing* na ngazi ya *Post graduate* ni 1, ngazi ya *Master* ni 4 ngazi ya *PhD* ni 1. Takwimu hizi kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti. Kwanza nakubaliana na maelekezo ambayo Mhe. Jaku Hashim ameyatoa katika hoja yake.

Lakini cha msingi Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mimi ningeliomba Serikali, naelewa juhudhi zilizofanyika hususan katika utawala huu tunaokwenda nao wa Dr. Ali Moh'd Shein katika kuwasaidia madaktari kutokana na kiwango chao walichokuwa nacho mwanzo cha maslahi yao hadi hapa kwamba sasa tumefikia.

Lakini bado iko haja na naomba jambo hili lizingatiwe vizuri zaidi, iko haja ya kuzidi kuangalia zaidi maslahi ya hawa madaktari hususan madaktari bingwa ambao wamekwenda masomoni na baadaye wakawa wanarudi katika visiwa vyetu nya Zanzibar kwa lengo la kuja kutusaidia Wazanzibari tulio wengi.

Mhe. Naibu Spika, sio siri kutokana na maslahi duni ambayo wanayapata madokta wetu hapa ndiyo chachu inayowasababisha madaktari wetu hawa kuweza kuamua kwenda hapa upande wa pili wa Muungano kwa ajili ya kuangalia maslahi mazuri zaidi na waweze kupata maslahi yao kwa ajili ya kuendeleza maisha yao.

Sasa pamoja na hali ngumu ya uchumi tuliyonayo naomba kuomba Serikali kwamba pamoja na manufaa na maendeleo ambayo wamewapatia madaktari hususan madaktari mabingwa bado iko haja ya kuangalia uwezekano mzuri zaidi wa kuendelea kuwaomba madaktari bingwa waweze kubakia hapa kwetu Zanzibar na waweze kupata maslahi kama vile wenzenetu watu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano ambayo wanayapata. Naomba hilo lizingatiwe sana.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana kwa asilimia 99 kwa hoja zote 7 au maazimio yote 7 ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub amekuja kutuelekeza katika hoja yake hii. Lakini zaidi Mhe. Naibu Spika, ningelipenda vile vile kuweza kumfahamisha kitu kidogo Mhe. Jaku Hashim Ayoub juu ya kipengele au azimio namba 4. Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu Azimio namba 4 kama linavyosomeka:-

" Serikali kuititia Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba fedha zinazotengwa katika Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia huduma za Afya zinaingizwa zote na kwa wakati, ili Wizara ya Afya iweze kutimiza wajibu wake kama ilivyojipangia."

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu hapa sioni kwamba pamoja na maslahi pamoja na bajeti ndogo vile vile inayopelekwa ndani ya Wizara ya Afya bado nahisi vile vile tunawajibu kama watendaji katika Wizara Afya kuhakikisha hichi kidogo pia kinachotiya ndani ya Wizara hii kitumike vizuri kwa sababu yako maelezo ambayo yanakuwa yanatoka kule kule kwa baadhi ya watendaji na baadhi ya watu wengine kwamba hata kile kinachotolewa vile vile kuna maeneo huwa hakifiki na kuna matumizi mengine ambayo yanakuwa hayalingani na ule uhalisia ambao umetakiwa. Ni wajibu wa Serikali kweli kuingiza fedha kwa mujibu wa uwezo wake. Lakini vile vile na ile fedha ambayo itakuwa inaingizwa na wao wizara wanapaswa kuwa makini kuhakikisha kwamba kile kidogo tulichonacho tunakitumia kwa manufaa ya wote.

Baada ya kwisha kumalizika kwa eneo hilo Mhe. Naibu Spika, ningelipenda vile vile kuelezea kipengele cha 6 ambacho nacho kinaelezea kwamba:-

" Wizara ya Elimu na Bodi ya Mkopo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wajiendeze katika mpango wa muda mrefu wa kusomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini".

Kipengele hichi Mhe. Naibu Spika, kinaoana kabisa na kile kipengele cha kule mwanzo ambacho nimezungumzia juu ya suala la kuwaenye na kuwaendeleza hawa madaktari mabingwa ambao wanatoka nje. Kwani madaktari hawa kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wanahuzunisha sana wanasomesha kwa jasho la wananchi Zanzibar wanapata misaada ya aina yote kwa kusaidiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Lakini baada ya kwisha kumaliza kupata taaluma zao wao wanaangalia maslahi zaidi baada ya kuangalia uwezekano wa kuwasaidia wananchi wa Zanzibar, lakini na wao pia madokta hawa ningeliwaomba vile vile pamoja na hali yao ya kuangalia maslahi zaidi ningeliomba vile vile uzalendo na wao wauweke mbele na vile vile Serikali itengeneze utaratibu makini na imara zaidi wa kuhakikisha kwamba hawa madaktri mabingwa ambao wanakwenda kusomesha nje wanaporejea hapa watengenezewa utaratibu kwamba hawatokuwa na uwezo wa kwenda kufanyakazi eneo jengine basi na kusaidia katika Serikali yetu na angalau kuweza kutumia yale matunda ambayo walikuwa wao wamesomesha kwa nguvu na fedha za wananchi wa Zanzibar ili waweze kusaidia katika nchi yetu na kuweza kusaidia kuleta maendeleo zaidi.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima mimi naunga hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa asilimia 99. Naomba kuwasilisha. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofii*).

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kutokana na umuhimu wa hoja hii ya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni nikaona na mimi basi nitoe mchangano wangu juu ya hoja hii na kama tunavyofahamu kwamba hoja hii inawagusa wananchi wengi sana au walio wengi ambao wanahitaji huduma za Afya, huduma bora kwa ajili ya maisha yao. Kwa hiyoo, ni hoja muhimu na ambayo inahitaji kuungwa mkono.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na hoja hii ilio mbele yetu na maelezo mengi yaliomo pamoja na *reference* nydingi ambazo Mhe. Jaku Hashim amezichukuwa kutokana na Bajeti yenye ya Wizara ya Afya ambazo zimekuwa zikitolewa katika bajeti mbali mbali naamini amefanya uchunguzi wa kina juu ya jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, suala la Afya ni suala muhimu sana na kwa sababu afya ndio kila kitu ukiwa unaumwa na ukiwa na afya mbovu maana yake huwezi kufanya chochote. Kwa hiyoo, taifa linahitaji watu wenye afya wenye uangalizi wa karibu, wanahitaji kupata huduma za afya zilizokamilika. Kwa hiyoo, ni hoja muhimu ambayo inahitaji kuzingatiwa. Nilikuwa nazungumzia na Mhe. Ali Mzee hapa na namuuliza mbona Waziri wa Afya ambaye leo tunazungumzia mambo yake simuoni yuko wapi au yuko kwenye kikao? Ananambia sijui tumpishana hapo nje lakini Naibu Waziri yupo, sawa Naibu Waziri yupo.

Lakini kitu kama hiki Mhe. Naibu Spika, ni *very sensitive* ambacho kinahitaji kama wewe ndie mwenye dhamana wa jambo hilo, sio amuache msaidizi wake tu na yeye ikawa anazagaazagaa nje. Tunajadili kitu muhimu sana ambacho kimegusa Wizara yake, asikilize Wawakilishi wa wananchi wanasesmaje juu ya hoja iliyo mbele yao. Mimi ninadhani kama kweli tupo *serious* Mhe. Waziri wakati wote alipokuwa kwenye Baraza hili alikuwa anazungumzia

juu ya *seriousness* ya Mawaziri. Wakati ule, alikuwa anawaauliza mara zote muko *serious*, Serikali iko *serious*. Sasa ninataka kumuuliza Waziri wa Afya yupo *serious* kwa sababu hoja hii tunayoizungumza hapa inagusa Wizara yake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja kwenye maazimio. Nitumie muda wangu mwingi kwenye maazimio kwa sababu maelezo ni mengi na yamejitosheleza; yana ukweli kwa kiasi kikubwa lakini hatimaye mto hoja amewasilisha maazimio ili Baraza hili liyakubali na liyapitishe ili sasa Serikali iyafanyie kazi. Hili ni eneo muhimu, tunaweza tukajadili, tukaenda lakini hatimaye Baraza hili kwa niaba ya wananchi sasa liazimie au liyakubali maazimio haya ili sasa Serikali ikayafanyie kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye azimio la kwanza Mheshimiwa Mto Hoja nitakuwa ninapenda kumnuuu-nukuu ili likae vizuri, anasema kwamba "Serikali ifanye mabadiliko ya kisera yatakayoizwesha Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu wetu nje ya nchi ili waweze kuwahudumia wananchi badala ya kutenga fedha nyangi ya kupeleka wagonjwa nje ya Zanzibar".

Azimio hili ni sahihi kwa sababu fedha ni kila kitu na ninakumbuka azimio la nchi za *SADC* limeazimia kwamba katika nchi wanachama wa *SADC* basi *atleast* watengene asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya masuala ya afya. Hili ni azimio la nchi zile zenye Umoja wa *SADC*. Sasa mimi nilikuwa ninajiuliza na ndio nilikuwa ninasema Mhe. Waziri atleast na ye ye angekuwepo, basi hebu Mhe. Waziri atakapopata nafasi atueleze kwamba sasa hivi katika bajeti hii ya mwaka huu ambao tunakwenda nao Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kwa jambo hili. (*Makofii*)

Kwa sababu hili ni azimio muhimu na kama tunavyojua fedha ni kila kitu na suala hili la kuwasafirisha wagonjwa wetu kwenda nje ya nchi ni muhimu, kwa sababu matibabu yanayopatikana katika hospitali zetu hizi hayatoshelezi yaani katika kuwahudumia wananchi. Tumeshuhudia kuna wananchi wengi ambao wanahitaji sasa kwenda nje kupata matibabu. Lakini na hili suala la kusomesha wataalamu ili sasa badala ya kwenda nje waweze kupata matibabu yao hapa; nalo ni jambo muhimu. Kwa sababu sote tunajua uwezo wa Serikali katika kuwasafirisha watu.

Takwimu hapa Mhe. Jaku Hashim Ayoub amezieleza na namna mitiririko mzima wa fedha zinazotumika kwa ajili ya kusafirisha kwenda nje ya nchi, lakini kuna idadi kubwa zaidi ya mara tatu, mara nne wale wanaohitaji hawapati fursa ya kwenda kule na matokeo yake wanapoteza maisha. Kwa sababu uwezo wa kutibu maradhi yao hatuna.

Kwa hivyo azimio hili mimi ninakubali kwa pande zote mbili; ama kwa upande wa Serikali kutenga bajeti maalum, si lazima kufuata azimio la *SADC* moja kwa moja lakini *atleast* basi kama nchi za *SADC* zimeweka asilimia 15 au ijapokuwa asilimia 10. Sasa ndio maana tulikuwa tunataka tujue kwamba mwaka huu bajeti yetu iko asilimia ngapi. Sidhani mimi kiwango hicho kimefikia. Kwa hivyo azimio hili mimi ninalunga mkono Hilo ni moja.

Jengine ni kwamba mabadiliko haya ya kisera yaende sambamba kuwa na mkakati wa kusomesha na wataalamu na fani ambazo zina upungufu hususan katika magonjwa sugu na mambo mengine. Nalo hili ni azimio zuri ambalo Waheshimiwa Wajumbe tunafaa kuliunga mkono ili sasa tupate wataalamu katika fani mbali mbali. Kwa sababu ukiangalia kiambatanisho hichi nambari 10 ambacho mto hoja amekiweka.

Kwa mfano, eneo hili la *ICU* ambapo taarifa hii Mhe. Waziri wa Wizara hii alipokuwa akiisoma mwaka 2012/2013, yaani ni bajeti ya mwaka juzi tu hii, ambapo inaonesha Kitengo cha *ICU*; mahitaji ya ma-nurses na ma-nurses ndio wanaokaa na wagonjwa mara zote. Juzi tulikuwa tunaambiwa hapa na Waziri wa Afya kwamba umuhimu wa wauguzi hawa na madaktari kwamba wauguzi ndio mara zote wanakuwa wanakaa na wagonjwa, lakini sasa hapa inashangaza kwamba *ICU* ina mahitaji ya wauguzi 24 na waliopo ni sufuri.

Mhe. Naibu Spika, sasa maeneo kama haya kwa takwimu hizi yanatutisha. Kwa hivyo, ni kweli ipo haja ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu wetu katika haya maeneo muhimu na mengine mengine ambayo siwezi kuyarejea hapa, lakini mengi yanaonesha sufuri mbali ya mapungufu. Inaonekana wataalamu hawa hawapo kabisa nchini kwetu. Kwa hivyo mimi ninakubaliana na azimio ambalo Mhe. Jaku amelieleza kwamba *atleast* Serikali itenye fedha kuwasomesha madaktari wetu, yaani watu wetu wasome katika haya maeneo muhimu ambayo yana upungufu.

Mhe. Naibu Spika, sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa naye kutoa maelezo yake, ninategemea atatoa maelezo basi *at least* atwambie haya mapungufu yaliyoonekana wakati ule wa mwaka 2012/2013 na sasa hivi hali ikoje. Lakini bado haja ya kuwasomesha wataalamu ipo ili wananchi wajue mapungufu yaliopo na hali halisi ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, azimio jengine ambalo Mheshimiwa mtoa hoja alilieleza kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya kimfumo wa kibajeti, kuanzia mwaka 2013-2016 utakaowezesha kupunguza kiwango maalum cha bajeti kinachotengwa katika sekta nyengine, ili kuweza kuongeza kiwango cha bajeti kinachotengwa kwa ajili ya sekta ya afya nchini. Hili ninadhani Mhe. Naibu Spika, nimeliunga mkono, maana limeowana na lile azimio la kwanza kwamba kuwe na bajeti maalum ambayo itawenza kusaidia kunyanya hali hii ya afya ya wananchi nchini.

Mhe. Naibu Spika, azimio la nne kwamba Serikali kuititia Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba fedha katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya zinaingizwa zote kwa wakati ili Wizara ya Afya iweze kutimiza wajibu wake kama ilivyojipangia. Hili nalo ni eneo muhimu Mhe. Naibu Spika, na kwa sababu afya ni kila kitu. Afya haiwezi kusubiri, mambo mengine yanaweza yakasubiri lakini afya ya binadamu akiumwa anahitaji apate huduma. Mgonjwa anapolazwa hospitalini anahitaji apate chakula.

Tumeshuhudia hapa wakati mwengine tunaambiwa bajeti imechelewa; bajeti za chakula zimechelewa, bajeti za huduma nyengine zimechelewa. Kuna maeneo lazima tuyape kipaumbele hayawezi kusubiri, hata kama hatuna lakini kuna maeneo ni lazima yapewe kipaumbele, kibajeti zake zitimie kwa mujibu wa zilivyo pamoja na upungufu wake.

Kwa hivyo mimi ninakubaliana na azimio hili nambari 4 kwamba Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba fedha hizo chache zilizotengwa zinapewa Wizara ya Afya kwa wakati, ili waweze kuwashudumia wananchi katika eneo hili. Hivyo, azimio hili ni sahihi nalo ninakubaliana nalo. (*Makofî*)

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kwamba Serikali imefanya mabadiliko ya mishashara na maslahi ya wataalamu wa afya *and so on*. Hili ni muhimu na tumekuwa tukilisema sana pamoja na juhudu ambazo zinachukuliwa na Serikali. Tunakubali juhudu imechukuliwa kubwa. Rais wa Awamu ya Saba Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein amefanya juhudu kubwa sana katika kipindi chake, amewawezesha madaktari kutoka eneo lililokuwepo na kuwasukuma sana kwa asilimia kubwa. Lakini bado juhudu inahitajika pamoja na ufinyu wa bajeti, pamoja na hali yetu ngumu ya kiuchumi, lakini eneo hili la afya ni muhimu kuliko maeneo yote.

Kwa hivyo maslahi ya madaktari, maslahi ya wauguzi, maslahi ya wafanyakazi katika sekta ya afya ni muhimu sana na ni lazima yaangaliwe, na sote tumeshuhudia jinsi madaktari wetu wanavyokwenda nje ya nchi kwenda kufanya kazi kutafuta maslahi mengine. Kwa hivyo ni vyema Serikali yetu tunajua wanajua umuhimu lakini waongeze juhudu zaidi ili kuona kwamba wale madaktari tuliokuwa nao tunawa-*handle* vizuri wasiende kututoka na wale waliokuwa nje basi wavutike kurejea hapa, kwa ajili ya kuja kuwashudumia ndugu zao na wananchi wenzao. Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo suala la maslahi ya wataalamu madaktari na wafanyakazi wa hospitali ni muhimu na Serikali inahitaji kuzingatia zaidi eneo hili kwa ajili ya wataalamu kuendelea kubakia katika kuwashudumia watu. (*Makofî*)

Mhe. Naibu Spika, azimio jengine na hili ninaliunga mkono ni kwamba Wizara ya Elimu, Bodi ya Mikopo ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwa kujieleza katika mpango wa muda mrefu wa kusomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini. Hili ninadhani nalo ni zuri na linakubalika na ninadhani hata utekelezaji wake linatekelezwa vizuri na Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu; kwamba wale madaktari wanafunzi amba wanaomba katika fani hii ya udaktari na mambo mengine, wanapewa kipaumbele kwa mujibu wa taarifa tulizokuwa nazo.

Kusisitiza juu ya jambo hili nalo ni muhimu kwa sababu wenzetu hawa wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu wasije tena wakaanza kutoka kwenda huku na huku, tunajua wana umuhimu katika mipango yao, katika sera zao eneo hili ni muhimu na wanatoa kipaumbele juu ya wale wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma udaktari na kupatiwa mikopo. Kusisitiza nalo ni muhimu na azimio hili ni muhimu, nalo ninaliunga mkono.

Mhe. Naibu Spika, mwisho azimio la mtoa hoja linasema Serikali iandae mkakati madhubuti na wenye kutekelezwa ndani ya muda mfupi kwa ajili ya kujaribu kuwarejesha nchini wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali

waliokimbilia sehemu mbali mbali duniani kwa sababu mbali mbali ikiwemo maslahi. Hili nalo ninaliunga mkono na njia pekee ya kuwarejesha ni ile ya kuboresha maslahi. Hiyo ndio njia pekee na kwa sababu Serikali mara zote hawazuii watu kwenda kutafuta maslahi zaidi nje, lakini wenyewe wakisikia kwamba sasa maslahi ya madaktari mazuri yanalingana na ya nchi nyengine, basi watarejea kuja kufanya shughuli hizi kwa sababu mtu ni kwao. Hichi kitendo cha kwenda nje huko kuhangaika kutafuta maisha ni namna tu ya kutafuta maslahi na maisha, lakini hakuna hata mtu mmoja anayependa kwenda kukaa nje ya nchi kuliko kukaa hapa ndani kushughulikia watu wao.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo kwa kweli mimi ninakubaliana na hoja zote ambazo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameziwasilisha mbele yetu. Maazimio yote, mimi ninakubaliana nayo ni muhimu sana ambayo Waheshimiwa Wajumbe tunahitaji tuyaunge mkono ili Serikali iweze sasa kuyaangalia na kuangalia zaidi namna gani wanaweza kuyafikia kulingana na hali ya uchumi wa nchi. Lakini pia waone na umuhimu kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tatizo letu sisi hapa Zanzibar tunakuwa na vipaumbele vingi. Tunaletewa bajeti hapa, unakuta vipaumbele vinane. Mimi siaona vipaumbele vinane; kipaumbele kinakuwa kimoja lakini unakuta bajeti inakuja hapa, unaambiwa vipaumbele vinane.

Sasa vipaumbele vinane hivyo tutavitekelezaje, hatimaye vipaumbele vinane miaka mitano yote inayokwenda hakuna kilichomalizika. Lakini unapoweka kipaumbele kimoja, maana yake unahakikisha nguvu zake zote unaelekeza pale mpaka unahakikisha lile ulilolikusudia linafanyika, ndio unachukua kipaumbele chengine.

Kwa hivyo, waweke kipaumbele katika sekta ya afya kwa sababu sote tunahitaji afya. Tumeshuhudia viongozi wetu wakuu hapa Mhe. Rais, Makamu wote wa Rais wanakuwa wanakwenda nje huko kwenda ku-check afya zao na matibabu. Kwa sababu eneo hili ni muhimu.

Mimi ninaamini kama tutakuwa na vifaa vya kutosha vya kisasa, hospitali za kisasa, hata viongozi wetu wakuu wangkuwa hawana haja ya kwenda nje huko kwenda kuangalia afya zao na kupata matibabu; wangkuwa wanatibiwa hapa hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hivyo eneo hili la afya ni muhimu kwa ajili ya wakubwa, wa kati na wadogo kwa sababu kila kitu ni afya. Humu Mhe. Naibu Spika, sidhani kama kuna Wajumbe wako hapa hawahitaji huduma za afya; sote sisi wabovu. Kama mtu hana hili ana lile, asiyekuwa na *pressure* ana sukari, asiyekuwa na sukari ana hili. Mhe. Saleh Nassor Juma ananiambia hapa akishahutubia hapa inabidi ameze vidonge. Sasa hiyo ndio hali halisi ilivyo. (*Makofi*)

Hivyo suala la huduma za afya ni muhimu sana. Kwa hivyo mimi ninaunga mkono azimio hili na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waniunge mkono. Lakini na Serikali sasa iazimie kuyaangalia haya maazimio kwa ajili ya manufaa ya watu wetu na mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu.

Wizara ya Fedha nayo haipo sasa, Waziri anayeshughulika na masuala ya fedha, kwa sababu hawa nao ni wadau wakubwa katika jambo hili. Waziri wa Afya hayupo lakini na Waziri wa Fedha pia hayupo, sasa wakati mwengine ndio yale tunayosema tunakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Unajua ukitwanga maji kwenye kinu Mhe. Naibu Spika, unatwanga maji kwenye kinu yanamwagika. Sasa sisi hapa tunatwanga maji kwenye kinu lakini wale ambao ndio wahusika wa mambo haya hawapo. Ndio maana wakati mwengine tunafika pahala tunajinyamazia kimya hatusemi.

Kwa sababu sio jambo zuri kwamba sisi viongozi tupo hapa tunazungumzia jambo muhimu, tunapoteza nguvu zetu, *energy* zetu, tunatoa mawazo yetu lakini wale wa kuyabeba yale wa kwenda kuyafanyia kazi wote hawapo. Tunaambiwa maana Serikali yote ipo, sio kweli kila mmoja ana jukumu lake hapa. Mhe. Ramadhani Abdalla Shaaban pale Serikali yupo, lakini anashughulikia masuala ya ardhi, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame yupo anashughulikia masuala ya utawala bora pale na Ikulu. Kwa hivyo Serikali ipo lakini kila mmoja ametwika dhamana yake. (*Makofi*)

Sasa mtu anaposema Serikali ipo, wewe sema tu. Kwa kweli sisi tunakuwa hatuna nguvu kubwa ya kusema, unaposema na yule mwenyewe anayehusika na sekta ile awepo; tunetegemea Waziri anayehusika na masuala ya fedha awepo, kwa sababu tunazungumzia juu ya kuiwezesha Wizara ya Afya kuweza kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa maazimio haya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. Ahsante ninakushukuru. (*Makofî*)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote ninadhani sitotenda haki kama sikufanya mambo yafuatayo;

Kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukiwa hai na hatimaye kutujaalia hazina ya afya njema na uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu mpaka katika jengo kubwa kama hili. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovoyote hatuna budi kumshuu.

Aidha, jambo la pili ambalo inabidi nilifanye ni kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi na mimi kuweza kusema lolote kuhusu hoja hii iliopo ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub mbele yetu. Kwa hivyo ninakushukuru sana.

Mwisho nimalizie jambo la tatu kwa kutoa pongezi za dhati kwa mleta hii hoja Mwakilishi makini, mahiri na anayejali sana afya na mdau wa Wizara ya Afya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Hivyo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi na vitongoji vyake ninachukua fursa hii kumpongeza sana kwa kuweza kuleta hii hoja. (*Makofî*).

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imechelewa sana kuleta, ilikuwa iletwe *day two* wakati baada ya kula kiapo anaileta, lakini amekaa karibu miaka minne ndio anatuletea jambo zuri kama hili! Lakini pamoja na hivyo kwa sababu limeshafika, acha tuseme seme maneno kidogo na kuitilia jalio hii hoja yako.

Mhe. Naibu Spika, hii hoja mimi nimeiangalia katika nyanja mbili. Nimeangalia kwanza nikiwa kama mdau upande wa afya, kwa sababu sote ni wadau wa hii hoja kudumisha ya afya. Upande wa pili wa hoja hii kwa sisi wachambuzi mambo ya kisiasa na kiuchumi, mimi nimeiangalia katika upande wa kiuchumi kwa sababu sisi Zanzibar ni nchi iliyokuwa haina viwanda; uchumi wake hautegemei viwanda. Zanzibar ni nchi ambayo uchumi wake hautegemei mafuta kama ilivyo nchi nyengine za *UAE* huko. Zanzibar ni nchi inayotegemea pesa za walipa kodi wa nchi hii. (*Makofî*)

Sasa mlipa kodi kama hana afya njema, basi usiutarajie uchumi wa nchi kama Zanzibar kama utakuja juu hata siku moja. Ndio siku zote unakutia kwamba ikiwa Zanzibar hatukuwajali wananchi wetu kiafya, basi tusitarajie kwamba kuna siku uchumi huu utakuja juu.

Sasa hii hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye kaiangalia kwa upande wa afya tu, lakini hii ni muhimu sana hata katika sekta ya kiuchumi wa nchi hii ya Zanzibar. Kwa sababu mwenye afya bora ndiye atakayelipa kodi bora. Kwa mnasaba huu nakupongeza vile vile Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Naibu Spika, msingi wa hoja hii ni hoja ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio, kuhusu uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa na wananchi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, huduma za afya hapa Zanzibar zimekuwa zikidorora na kuzorota siku hadi siku. Sababu ni ipi inayosababisha afya za wananchi kuzorota zorota hivi. Mimi nadhani sababu zinaweza kuwa kama zifuatazo. Kwanza kama alivyoeleza mwenyewe Mhe. Jaku Hashim kwamba bajeti ndogo.

Mhe. Naibu Spika, uhaba wa bajeti wa wizara hii ni msingi mmoja ambao unasababisha kwamba *wa-meet zile demands* za wizara. Kwa mnasaba huo mambo mengi yakashindwa kutekelezeka na kwa hivyo kuona kwamba hali ya afya inadorora kwa sababu ya bajeti ndogo wanayopewa hii wizara.

Kuna nchi Waheshimiwa Wajumbe inatumia karibu asilimia 60 ya bajeti yake kwenye afya. Sasa hiki kinchi chetu sisi, sidhani kama hata asilimia 40 inafika ya *total budget*. Lakini hicho kidogo hakikamilishwi, kama alivyotoa katika maelezo yake hapa Prof. Jaku Hashim Ayoub. Sasa Mhe. Naibu Spika, hii ni sababu moja kwamba hata bajeti ya nchi haitilii maanani afya. Sababu ya kwanza hiyo.

Sababu ya pili ni tuseme ni uhaba wa madaktari au vifaa vya kuchunguza afya. Mimi sidhani kama tuna uhaba wa madaktari hapa. Lakini madaktari wapo, lakini sasa kutunzwa kwa madaktari hawa ndio tatizo. Hawatoshi, lakini hawa waliopo hawatunzwi.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana. Mimi nilikuwa najua siku zile tulikuwa na *specialist* katika mambo ya *psychiatric* Dkt. Wakili, yule mzee kajitahidi sana kutibu hapa na sasa hivi utakuta tatizo la wagonjwa wa akili ni kubwa, *specialist* tuliyekuwa naye ni Dkt. Wakili, kastaafu nadhani kwa sasa. Serikali ikapapatua papatua wamepata *specialist* mmoja anaitwa Dkt. Khamis, huyu Dkt. Khamis Othman ye ye yuko pale kama *psychiatric* lakini anatunzwa vipi. Mimi ninaye mmoja tu, huku idadi ya wateja inaongezeka, kwa hivyo mambo ya mitaa yanaongezeka. Lakini *specialist* tulienyaye sasa hivi naona ni mmoja tu. Akiondoka Dkt. Khamis hakuna *psychiatric* pahala hapa. Mimi nadhani tuwatuunze.

Mimi nakumbuka kuna *specialist* mmoja, *pediatrician* mmoja anashughulika na magonjwa ya watoto. Yuko Dar es Salaam katika taasisi moja, ni *specialist* huyo. huku alikuwa akilipwa shilingi 700,000 kwa mwezi, kule anapewa shilingi milioni 2,000,000 hayupo kaondoka, yaani hatuwatuunzi madaktari na sababu ni hiyo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tuangalie kwenye maazimio ambayo amesema Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Azimio la kwanza. Maazimio yote kwanza naunga mkono. Lakini mimi nitafafanua zaidi katika azimio namba tano, kwamba serikali ifanye mabadiliko ya mishahara na maslahi ya wataalamu wa afya, ili kuwapa moyo wataalamu wetu na hivyo kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Lakini pia kuwa na maslahi mazuri yatakayopelekea wataalamu hao kubaki nchini na kuwashudumia wananchi. Hili nimeshalifafanua, kwamba maslahi ni muhimu na ndio maana ma- *specialists* wanaondoka, maslahi sio pamoja na mishahara tu, lakini pamoja na marupurupu mengine.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa muuguzi wa afya maslahi yake ni madogo sana, hawa ma-*nurses* ni madogo sana na wanafanyakazi katika *risk*. Kuna wagonjwa watoto wao wanashindwa kuwauguza, watoto wao waliowazaa wanawaogopa kuwafika, wazee wao waliowazaa wanawaogopa kuwafika kwa maradhi yaliyoingia. Lakini *nurse* anakwenda pale anamu-*handle* katika mazingira magumu sana. Maana yake hivi sasa japo kunyanyapaa imekatazwa, lakini mpaka sasa hivi unakuta mzazi anajifungua pale huku akiwa ni *positive HIV*, kwa wanamuogopa kumu-*handle*, lakini *nurse* hapa anamu- *handle* katika hospitali. Sasa kwa nini asilipwe maslahi ya kuweza kufanyakazi katika mazingira kama yale ya *risk environment*. Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub nadhani katika hili umesibu na mambo haya naiomba serikali iyaangalie sana.

Kuna ma-*specialists* katika mambo ya *surgery*, ma-*sujuniors* hawa, wanakwenda wakirudi katika *theatre* kumfanyia operesheni mgonjwa aliyekuwa ana *HIV*, akijichuna kidogo na kile kisu walichomfanyia, basi na ye ye kaganda. Hii ni hatari mazingira hatuyaangalii ya hawa madaktari wetu, sasa wasitukimbie. Wakati akienda katika Hindumandal *Hospital* pale akiingia katika *normal* operesheni mbali na mishahara anapewa *surgical allowance* ya kutosha, watatukimbie tu hawa sisi. Ati hawana uzalendo, uzalendo wanaao, mbona hawabidilishi uraia, uzalendo wanaao. Hata nyinyi Wawakilishi hapa mnapofikwa kuguswa katika maslahi yenu mnakuwa wakali sana. Sasa wao hata wakisema hawasikilizwi, je wasikimbilie kwenye maslahi mazuri! Watakimbilia tu.

Mimi naomba tuboreshe maslahi ya ma-*specialists* wetu, ma-*nurses* na wafanyakazi wote wa kada ya afya. Kinyume na hivyo afya itaendelea kuzorota siku hadi siku na uchumi wa nchi utaendelea kuwa mdogo hapa, kwa sababu taifa linakuwa na watu waliokuwa hawana afya.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kwamba Wizara ya Elimu na Bodi ya Mikopo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, wajielekeze katika mpango wa muda mrefu wa kuwasomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini. Ni kweli wanajitahidi bodi ya mikopo hapa. Lakini wanachopewa ni kidogo, serikali haitengi fungu kubwa kwa ajili ya kuwasomesha. Mimi nadhani katika hili Mhe. Naibu Spika, lazima serikali iwe *serious*. Pamoja na kwamba tunacho Chuo cha *School of Medicine*, lakini mimi naona kwamba lazima bodi ya mikopo iongeze uwezo wa kusomesha, tena itowe kipaumbele katika mambo haya ya madaktari.

Nashukuru kwamba mpaka pale Prof. Rai na bodi ya ufundu, ile *technical bench* ya SUZA wameshaanzisha na wao *First Degree in Medicine*. Kwa hivyo, mimi nadhani ikiwa tutaiwezesha Wizara ya Elimu na Bodi ya Mikopo wakapewa pesa za kutosha, basi wataalamu tutakuwa tunazalisha hapa hapa, sio lazima tupoteze mamilioni ya

mapesa kuwapeleka wagonjwa wetu India, na sehemu nyengine wapi huko. Hapa hapa tuna wataalamu hao hao kina Dkt. Jidawi ambae pia ni Katibu Mkuu pale, anajitahidi katika masuala ya kupasua watu pale. Sasa mimi naamini kwamba vyuo vyetu tukishawasomesha wale vijana, chini ya uongozi wa *bench* ya ufundi pale katika Wizara ya Afya watafanyakazi vizuri na badala ya kuwapeleka India tutawafanya hapa hapa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, serikali iandae utaratibu wa kuwarejesha. Kuwarejesha hapa nawaambia mimi itakuwa ni kazi, lakini tujitahidini tu watarudi hapa. Pale Dubai katika Rashid Hospital pana vijana wa Kizanzibari wasiopungua 15, *University ma-specialists* katika fani mbali mbali pale, lakini wanalipwa Diriham 20,000, 25,000. Sasa huyu ukishamboreshea maslahi yake kwa *rate* za hapa naamini uzalendo utakuwa na watarudi tu.

Mwisho nimalizie Mhe. Naibu Spika, kwamba sisi tunaangalia kwa madaktari na watu wengine wa sekta ya afya. Lakini vile vile tuangalie vifaa nya afya katika nchi yetu, ambavyo vinarudisha nyuma huduma ya afya kukosekana kwa vifaa nya afya.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba mpaka hivi sasa tangu mwaka 1964 tulivyopata uhuru hadi leo hii, tunakuwa na tatizo linaloongezeka sio Ukimwi tu unaoongezeka katika nchi hii. Lakini kunaongezeka maradhi haya ya *cancer*, kwa sababu ya hayo malaji. Alisema Mhe. Naibu Waziri wa Afya hapa asubuhi, mfumo wetu wa maisha, wakati anajibu swali langu pale. Mfumo wa maisha unatusababishia kuwa na matatizo ya afya sana, likiwemo hili la *cancer* na kila kukicha mambo yanazidi, kwa sababu haya mavyakula tunayotumia *cholesterol* chapa chapa iliomo katika mafuta haya tunayokula.

Sasa mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, katika hili, napata aibu sana kwamba nchi kama ya Zanzibar iliyopata uhuru wake mwaka 1964 tena sio kwa kusema sema maneno tu, hapania; tumepata uhuru wa aina yake sisi Zanzibar, sio wa kukaa majukwaani kina tukisema maneno, hapania. Ni uhuru mgumu wa kujisifia katika mambo ya siasa mbali mbali za kilimwengu. Leo sisi tunashindwa na mpaka sasa *Ocean Road* ndio wanaofanya *treatment* ya *cancer*. Sisi tokea mwaka 1964 mpaka leo hii hatuna mashine za kupimia saratani. Si aibu hii! Ni aibu kwa sisi nchi inawotuumu ni aibu kubwa kushindwa.

Sasa naiomba serikali Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameibainishia serikali, katoa tanbihi. Mhe. Jaku Hashim ametoa tanbihi kwa serikali, muwe makini katika kudumisha afya ya binadamu, ni pamoja na kutuletea mashine za kupima hapa hapa, sio kila mtu akipata saratani hata ya kidole tu akimbilie *Ocean Road* jamani kwa nchi kubwa kama hii.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuhusu mashine ya *DNA*. Siku zote hapa tulikuwa tukiambiwa na Waziri wa Afya aliyeondoka kuwa *DNA* tuna mpango huu na huu, muda umekuwa unamalizika wa awamu hii tena. Huu muda unamalizika hiyo *DNA* mashine, sio kwamba itatusaidia kwa afya tu, lakini hata katika mambo ya utawala bora ile *DNA* itatusaidia, kwa sababu makesi mengi ya mambo ya kudhalilisha, kina mama kesi nyingi zinaganda kwa sababu ya mashine ile ya *DNA* haipatikani. Basi mbali ya kuwa inasadida afya, lakini itassaidia kina mama wanadhalilisha na watoto wanadhalilishwa. Hivi meli imenunuliwa kwa mabilioni. Jamani ndio tuje kushindwa na mashine za kupimia saratani na *DNA*, mashine miaka yote hii, hamna kipaumbele serikali, hili ni tatizo kabisa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimalizie tu kwamba nilipoiona hoja hii nilikuwa nakumbuka yale matunda ya Mapinduzi, elimu, afya na maji. Naamini Marehemu Mzee Abeid Amani Karume angekuwa hai katika nchi hii, basi afya ingekuwa bure na *DNA* mashine ingekuwa imeshakuwepo hapa Mnazi Mmoja na Wete. Hebu jamani endeleseni dhamira ya Mapinduzi ya mwaka 1964, kwa kuwapatia afya bora wananchi, tena iliyokuwa ya bure kabisa. Hata kuchangia sasa maisha yamepanda, lakini mambo kama haya ya *DNA machine*, mambo kama haya ya kupimia saratani. Kusaidiwa na hao Tanganyika, ambao Tanganyika wenyewe TV ya rangi walikuwa hawajaipata, tuliipata sisi tunajidhalilisha sana. Ahsanteni sana naunga mkono na naunga mkono maazimio yote haya. Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri Wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii. Naomba kwanza na mimi nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwepo hapa tukijumuika na mwenzetu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye amekuja na hoja muhimu sana, nayo ni kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio. Narudia tena Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio kuhusu uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa kweli mimi nimesimama hapa kutoa mchango wangu kwa maazimio haya ambayo amekuja nayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naamini kama kutakuwa na kauli ya serikali maalum, basi itatolewa na wahusika wa serikali ambaye ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ndiye mwenye kutoa kauli ama Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kutokana na kanuni za Baraza la Wawakilishi juu ya kauli ya moja kwa moja ya serikali.

Lakini mimi mchango wangu zaidi utajikita upande wa Wizara ya Afya na juu ya maazimio haya. Naomba kabisa kwa dhati nimpongeze sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hasa kwa kianzio chake cha mwanzo alichoanza, ambacho nitaomba ninukuu kwenye hoja yake.

"Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais wake Dkt. Ali Mohammed Shein, imekuwa na malengo ya dhati kabisa ya kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wake, ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kulijenga taifa lao".

Naamini kama Mhe. Rais anasikiliza hili, basi naamini Mhe. Rais pia atachukua hatua adhimu ya kumpongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa kauli hii. Kwa kweli ni kauli nzito, ameanza hoja yake ya maazimio vizuri na ameanza moja kwa moja, naweza kusema kwa kuipongeza serikali kwa jitihada zake na juhudhi zake ambazo imekuwa ikichukua hadi hapa ilipofikia sasa.

Anaendelea kwa kusema kwa kuwa "...kuhakikisha kwamba lengo hili linatimia. Serikali imekuwa na sera, sheria pamoja na mikakati mizuri ya kuwapatia wananchi huduma bora za afya". Juu ya hili serikali haikubaki nyuma hata kidogo na ninamshukuru sana Mhe. Jaku Hashim analitambua. Ingawa Mhe. Saleh Nassor Juma amesema imechelewa sana, lakini *better late than never*, bora kuchelewa lakini ufile ile safari.

Kwa hivyo, mimi naweza kusema imekuwa muda muafaka pia, kwa sababu sera sheria zote zimekamilika na anatoa changamoto ya kuyatimiza yale ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya malengo yake ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ilianza.

Kwa kuwa serikali inaelewa kwamba maendeleo ya nchi yote yanategemea nguvu kazi za wananchi wake, ambayo inapatikana kutoka kwa wananchi wenye afya iliyomara. Kwa hivyo, haya yote kwa jumla kwa kweli yanaunga mkono dhamira iliyokuwa nayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Kiongozi mahiri Dkt. Ali Mohammed Shein ambaye leo hii naweza kusema katika hotuba yake aliyoitoa juzi, Chuo cha Afya Mbweni pamoja na siku ile ambayo madaktari waliokuwa wakisoma, madaktari wetu wenywewe, watoto wetu wa Kizanzibari waliokuwa wakisoma pale chini ya Universidad Nacional de La Matanza ya nchini Cuba; basi Dkt. Ali Mohammed Shein alisema, kwamba hivi sasa kutokana na idadi ile ya madaktari kuongezeka basi kuna haja huko mbele tunakoeleka tupate madaktari ambao watakuwa na *specialization*.

Nikisema *specialization* ndio taaluma hizi Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizozitaja katika maazimio yake kwenye kiambatanisho Namba 10, ambayo inazungumzia hali halisi ya mahitaji ya wafanyakazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane naye Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba kweli *deficit* ipo. Hivi sasa kidogo nitaondoka kwenye sekta ya afya nitazungumzia kama mchumi au sekta ya uchumi, maana na huko kidogo nilidokoa hapa na pale.

Wakati Mhe. Waziri wa Afya anawasilisha hotuba yake katika bajeti iliyopita pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha, wakati huo nilikuwa *backbencher* nilikuwa nikichangia kama mchangiaji mwengine na kama anavyofanya Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Kwa hivyo, nilimuuliza na kama *hansard* itatafutwa basi itaonekana kwamba nilimuuliza Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tuna mbinu gani wakati huo; mbinu gani ya kuangalia kuzalisha zaidi kuliko matumizi. Kwa mfano, Wizara ya Elimu ni wizara ya matumizi ni *net fender*, Wizara ya Afya ni wizara ya matumizi ni *net fender*, lakini kuna wizara za kuzalisha kama vile Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na wizara kadhaa nyengine za kuzalisha.

Sasa katika uchumi kitu cha mwanzo kabisa unaambwa kabla hujatumia kile ulichokuwa nacho upange kuzalisha *there is no expenditure without revenue*, yaani bila ya kuwanacho huwezi kutumia, utakopa utafanya kila kitu, lakini bila ya kuwanacho huwezi kutumia.

Kwa hiyo, hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha iliweka wazi na mahesabu yote tuliyofanya kwa kitabu cha bajeti iliweka wazi kwamba Zanzibar tuna-*deficit* ya asilimia 60, upungufu ambao unajazwa kutoka ile asilimia 60 kutimiza kidogo unashusha unafikia upungufu wa asilimia 45, wizara zote husika. Hivyo, hata kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub atapitia tena katika hotuba ya Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara nyengine zote atagundua baadhi ya sehemu kuna *deficit* kati ya asilimia 60 mpaka 45 hazijapata kasma zake katika zile idara.

Sasa nilisema na nitarudia tena leo kwamba tuna kila sababu ya kuwapongeza watendaji, watoa huduma, wauguzi, wakunga wa Wizara ya Afya kwa hapa tulipofikia na nitaleleza sababu gani. Kwa kweli tunawapongeza kwa moyo wao wa kizalendo wa kujitolea zaidi, kwa sababu hawafanyi kazi kwa mshahara tu, isipokuwa wanafanya kazi kwa moyo wa kujitolea ambao ni wa kizalendo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa mifano michache ambayo itathibitisha kauli yangu hiyo. Hivi sasa vijana wetu wanaosoma udaktari kutokea wale ambao wanafadhiliwa na serikali na wale pia waliokwenda binafsi ambao wazee wao wanawafadhili wako wengi siku hizi; wako waliokwenda China na zamani ilikuwa China ni serikali tu ndio inapeleka wanafunzi kwenda kusoma China, siku hizi hata mtu binafsi anapeleka na wanazo ofisi zao mbali mbali ambazo zipo hapa nchini kazi yake ni kuwatafuta wanafunzi kwa ajili ya elimu ya juu.

Kwa hivyo, wapo waliokwenda China, tena ni vijana mbali mbali kutoka Zanzibar ambao wanaosoma nchini Ukraine, wako wanaosoma Uturuki katika ile *scholarship*.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kitu kimoja kwamba daktari aliye maliza *degree* yake akapasi vizuri akitua Dar-es-Salaam mshahara wake si chini ya milioni mbili na nusu, yaani unaanza milioni mbili na nusu kwenda juu. Kwa hiyo, inataka daktari mwenye moyo wa kizalendo kweli kweli kuacha mshahara kama ule shilingi milioni mbili na nusu kwenda juu na hapo bado hujapata *specialization allowance* ukaacha ukasema mimi nakwenda kuitumikia nchi yangu kwa mshahara wa shilingi laki nane.

Kwa maana hiyo, daktari huyo anaacha shilingi milioni mbili na nusu anakuja kufanya kwa mshahara wa shilingi laki nane au tisa hawajafikia hata kiwango hicho wengine, basi hapo wanahitaji kupongezwa sana kwa moyo wao wa kizalendo kwa kujitolea kwa nchi yao na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawalipa kwa mema ambayo wanatutendea sisi.

Mhe. Naibu Spika, hapa katika hichi kiambatanisho inaonesha hali halisi na mahitaji ya wafanyakazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kweli anachosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub na hizi ni data ambazo zimetolewa katika hotuba ya Mhe. Waziri ambayo iliyotolewa hapa Barazani.

Vile vile naomba nikiri kwamba hii ndio ile inayochangia kwenye *deficit* ile niliyoelezea kama mchumi katika Wizara ya Fedha asilimia 60 ndio hii *deficit*, hii kwamba maeneo mengine yanakuwa mabaya sana unakuta mtu *zero*. Kwa kweli wanahitajika watu 10 katika *Psychiatry*, lakini hapa kuna *zero*, kwa hiyo *deficit* ama upungufu ni wote 10.

Kuna idara nyengine kama mfano nitachukua idara muhimu zile za *Oncology* na Mhe. Saleh Nassor Juma alichangia hapa masuala ya *cancer* au saratani. *Oncology* ni masomo haya ya saratani wanahitajika watu 9 na tumeelezwa hapa katika jaduweli hili ambalo Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliloliwasilisha hapa, lakini tuna *zero*.

Kutokana na hali hiyo, leo na ndio sababu ikawa watu wanakwenda pale *Ocean Road* hata kwa kipimo kidogo kabisa, kama vile kipimo cha *mammogram* mwanamke kupimwa ziwa lake, yaani ni kipimo ambacho ni kidogo kabisa. Basi kwa kipimo kile ambacho kinaweza kufanya kifa hata kwa *self examination* mwanamke inabidi atoke hapa agharamie nauli pamoja na mambo yote kwenda pale na wala sio kwa sababu kile kifaa hatuwezi kununua. Kwa kweli, bei yake sio ghali sana kifaa kile lakini kinahitaji taaluma kubwa sana ya kukiendesha, kukisimamia na *nurse* yule wa *Oncology* kuweza kutoa huduma ile kwa wagonjwa.

Mhe. Naibu Spika, *Oncology* ni katika *field* za afya siku hizi ambayo ni *very demanding*, yaani ina mahitaji makubwa sana ya soko. *Oncology Nursing* au *Oncology*, yaani Daktari basi analipwa mshahara zaidi kuliko kada nyengine, kwa hiyo hawa hata huko *Ocean Road* kwenyewe wanawatafuta. Kwa hivyo, mapungufu yapo na mapungufu mengi zaidi ni kutokana na bajeti na hali ya fedha hilo linajulikana.

Sasa hapa hatua tuliofika na hatua ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikia na kwa bahati nzuri Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein anatokea katika *field* hiyo hiyo juzi amepewa zawadi kubwa kabisa, ambapo amechaguliwa kuwa mtaalamu bingwa katika ile *field* yake ya mambo ya *laboratory* au *microbiology* na Chama cha Madaktari Bingwa cha Afrika nzima, ye ye amezawadiwa Shahada ya Heshma ya Juu kabisa. Tunampongeza kwa hilo na ninaamini kuwepo kwake ye ye sekta ya afya na maazimio haya yaliyoletwa yataweza kuimarika zaidi. (*Makofî*)

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuchangia katika ukurasa wa pili naomba ninukuu juu ya maelezo ya hoja anasema Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye amewasilisha hoja hii "Na kwa kuwa sisi, viongozi na wawakilishi wa wananchi, tunazishuhudia na kuziona jitihada hizi ambazo zina azma ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na hivyo kupasa kuziunga mkono". Mhe. Naibu Spika, namshukuru kwa hilo na sisi tunaendelea kuziunga mkono na mimi naunga mkono maazimio haya. (*Makofî*)

Kabla sijamaliza nina mawili matatu ya kuongezea. Mhe. Naibu Spika, ni kweli Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali amechangia hapa kwamba, kweli Wazanzibari wako wengi duniani, lakini si rahisi kuwaleta wote wale hapa na wala si rahisi ku-*afford* kuwalipa wote hawao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alikuwa anajibu swal la meli hapa, kwamba tulipotaka kununua meli karibu wizara zote zilitatwa humu ndani, yaani bajeti zote katika *other charges* pamoja na mambo mengine kwa ajili ya kutaka kununua meli tu. Kutokana na hali hiyo, kila wizara ilitakiwa kuchangia na ilikatwa mkato fulani kutoka bajeti yake ndio maana leo Waheshimiwa Wawakilishi wamekuwa wakiuliza sana masuala ya meli.

Kwa hiyo, hali halisi tuelekee kwenye kuzalisha zaidi. Sasa wazo lile la kuundwa kamati sio ya Baraza la Wawakilishi, isipokuwa ni kamati ambayo itatokana na Baraza la Wawakilishi kwenda sehemu tofauti kujaribu kutafuta ile *deficit* iliopo hapa, ili kupunguza baadhi ya mambo yaweze kufanyika hapa hapa.

Kwa kweli, naona wazo hilo sio bayaa ni zuri kama hiyo kamati itaundwa na ye ye mwenyewe akiwemo Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, basi wanaweza kwenda kwa Wafalme tofauti. Kwa mfano, Qatar, Ras-el-Kheima, Abudhabi, Dubai na kwengineko na Waheshimiwa Wajumbe nao wakapata nafasi hiyo ya kuungana naye. Nasaidiwa majina mengine ambayo siwezi kuyataja hapa, lakini ni majina ambayo yanajulikana.

Kwa hivyo, kwenda pale na kujaribu kuzungumza nao vizuri na ninaamini Mhe. Naibu Spika kama kitie chako kitatoa barua rasmi yenye nembo ya Baraza la Wawakilishi, basi lazima matokeo na majibu yatakuwa mazuri sana.

Wakati huo huo Mhe. Naibu Spika, kuna zile nchi ambazo zilizoendelea duniani nilikuwa naangalia kwenye *internet* kidogo, yaani zenye *federal reserve* kubwa sana na nchi hizo nitazitaja ambazo takribani ziko 10; nyingi mionganii mwao zinasaidia Zanzibar na hasa zinasaidia sekta ya afya moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa katika *federal reserve* ya ulimwengu ni Norway, yaani hawa wana *surplus* kubwa sana ikifuatiwa na Qatar nayo ina gesi na mafuta na nchi nyengine mbali mbali kama vile Denmark, Sweden, Finland, Switzerland, Abudhabi zote hizi kupitia zile *funds* zao, kwa hiyo hizo ninaweza kusema ni nchi ambazo zinaweza kushajihishwa zaidi.

Kuhusu kwenda kuwatibusi wagonjwa nje; jambo hili Mhe. Naibu Spika, kwa sasa tunaweza kutumia mbinu kadhaa kuliepuka, ili tunachopeleka kama wizara ni wale wagonjwa ambao wanahitaji mahitaji yale ya kwenda kutibiwa nje.

Kwa kweli, tukiziangalia bajeti kama alivyoziwasilisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub hapa kama hii 2.5 bilioni bajeti ile tungeweza kuitumia kwenye masuala mengine hapa hapa kwa ajili ya kufanya maendeleo ya sekta ya afya, ili

wagonjwa wasiweze kwenda kutibiwa nje kwa kweli lile tungeweza kulifanya. Sasa kwa kuwa maradhi mengine kwamba hatutibu hapa moja kwa moja na ni muhimu ndio maana inabidi tuyafanye hayo.

Kwa kumalizia kabisa Mhe. Naibu Spika, nataka kuzungumzia masuala ambayo alizungumzia Mhe. Saleh Nassor Juma na kuyaunga mkono baadhi yake kuhitaji *specialist* na *specialization* kunahitajika kweli. Sasa wengi wakipelekwa kusoma habati nzuri wengi wao wanarudi na wengine wachache wanabakia huko huko kwa sababu manufaa yanakuwa makubwa zaidi na michango inakuwa mizuri zaidi kule na marupurupu yanakuwa mazuri zaidi, kwa hiyo wanatafuta *green pasture*, yaani sehemu ambazo zilizobora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, haya yote yaliyozungumzwa kuhusu upande wa mashine tunaendelea nayo. Mhe. Naibu Spika, sisi tunazo mashine nyengine pale hospitali hata wataalamu wakuzitumia mashine zile hatuna, yaani kuna mashine kama tano mpaka sita na ninaweza kuwasilisha orodha hapa.

Kwa mfano, hii mashine yetu ya *CT-Scan* ambayo tumeitengeneza juzi basi sisi tunahitaji angalau tuwe na *radiographers* wanne na sasa tunao *radiographers* wawili tu na mmoja ni mtaalamu kutoka China na mwengine ni wa hapa yaani mzalendo. Pia kuna *radiographer* mmoja aliyekwenda kusomeshwa aliporudi tu Hospitali ya KCMC yenye imemtaka na imebidi aende huko kutoa huduma nako, kwa sababu unajua tena Mhe. Naibu Spika.

Kwa hiyo, mimi kwa upande wa maazimio haya yaliyotolewa naomba kuyaunga mkono maazimio haya kuhusu uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi.

Baada ya maazimio haya Mhe. Jaku Hashim Ayoub atakapokuja mwenyewe kujumuisha pale nitamuomba afanye jambo moja, yaami baada ya kuchukua maazimio haya kutoke na kitu chengine, yaami kuundwa kwa kitu kidogo kama *taskforce* hivi ambayo itakuwa kila panapotokezea jambo pakahitajika mashine au huduma fulani kama vile mashine ya kupimia *cancer* au *DNA* kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma.

Kamati ile itakayotokana na maazimio ya Baraza inaweza ikatumwa hasa na Baraza kufanya mazungumzo na nchi mbali mbali au na wafalme tofauti ama viongozi mbali mbali kwa ajili ya kusaidia sekta ile moja kwa moja, kwa sababu maazimio yale ndio na yale ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, yatakuwa yametimia pamoja na maazimio ambayo yapo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar moja kwa moja tokea mwaka 1964 juu ya sekta ya afya na elimu. Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono maazimio haya yaliyowasilishwa. (*Makofit*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Sasa tunampa nafasi kidogo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naye aseme machache. (*Makofit*)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kusema machache katika hotuba ama maazimio ambayo Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameyaleta mbele ya Baraza hili.

Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa dhamira yake njema katika suala zima la kusimamia sekta ya afya. Kwa kweli, humu ndani sote tunamuamini sana kwamba amekuwa mfano bora katika kutazama au kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya sekta ya afya, jambo ambalo sote tunaliunga mkono kuona kwamba afya za watu wetu zinaimarika na zinakua vizuri. (*Makofit*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub amekuja na maazimio saba, maazimio ambayo ukiyatizama kwa undani tayari serikali imeanza kuyafanya kazi na inayafanya kazi kutokana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Vile vile kuona umuhimu wa sekta nyengine katika suala zima la kusimamia shughuli za serikali na nchi kwa ujumla wake.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika azimio lake namba 1 naomba nilinukuu anasema "Kwamba serikali ifanye mabadiliko ya kisera yatakayoiwezesha serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu wetu nje ya nchi, ili waweze kuwashudumia wananchi badala ya kutenga fedha nyingi kwa ajili kupeleka wagonjwa nje ya Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea kufanya hivyo na imekuwa inajitahidi kadri ya uwezo uliopo kusomesha vijana wetu, ili wawe na taaluma kubwa katika kutoa huduma za afya na itaendelea kufanya hivyo. Kwa hivyo, hivi sasa sera hiyo ipo na utaratibu wetu wa kuendelea kutoa huduma kwa wagonjwa waliopo, kwa sababu huwezi kuwa na mgonjwa yupo mbele ya macho yako hivi sasa kwamba anaumwa ni mgonjwa ukasema usimpeleke katika matibabu.

Tuta-*commit suicide* imesababisha wengine ambao matibabu yao hayawezi kupatikana hapa lazima yapatikane nje, basi hatuna budi na wananchi wetu wengine hali zao ni za kipato cha chini, hivyo natuna budi kuchukua hatua ya kuwapeleka nje kwa ajili ya kuwafanyia matibabu. Kwa hiyo, bajeti ambayo tunaifanya sasa bado ni ndogo kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wetu.

Kutokana na hali hiyo, bado tuna *challenge* hapa Mhe. Naibu Spika, kwamba ukisema uzichukue fedha ambazo za wagonja ambao tungeweza kuwatibu na uache kuwatibu na uanze kuwasomeshea wataalamu ni tatizo gumu kidogo.

Hata hivyo nakubaliana sana na hoja ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya pale aliposema suala zima la kuzidi kuimarisha uchumi wetu, ili kujenga uwezo mkubwa zaidi kwa nia na madhumuni ya kuwawezesha vijana wetu kupata taaluma zaidi katika hii sekta ya afya. Jambo hilo lina umuhimu wake na serikali itaendelea kufanya hivyo kwa msingi wa kuendeleza huduma za afya na kuwasomesha watu wetu. Sasa ukisema upunguze bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa ambapo hivi sasa haitoshi itakuwa pia nalo ni tatizo.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni azimio la 2 Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema kwamba, mabadiliko hayo ya kisera yaende sambamba na kuwa na mkakati wa kusomesha kwa awamu wataalamu wa fani ambazo zina upungufu, hususan katika magonjwa sugu yanayaoshindikana kutibiwa ndani ya Zanzibar na kuacha kujikita katika kusomesha wataalamu katika fani hizo kwa hizo ambazo tayari zina wataalamu wa kutosha.

Hoja yake hii ina msingi mkubwa na mimi nataka nikubaliane nae moja kwa moja kwamba umuhimu wa kusomesha vijana wetu katika maeneo hususan ambayo magonjwa yamekuwa mengi na magonjwa sugu, hilo ni jambo halina mjadala na jitihada hizo Serikali itanedelea kufanya na ushauri huo tunaupokea.

Hoja ya tatu kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya kimfumo wa kibajeti kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 utakaowezesha kupunguza kwa kiwango maalum cha bajeti zinazotengwa katika sekta nyengine, ili kuweza kuongeza kiwango cha bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya afya nchini, Mhe. Spika, hivi sasa tunachokifanya moja katika eneo la kipaumbele *priority area* ni Wizara ya Afya. Tutaendelea kufanya hivyo lakini huwezi ukasema na sekta nyengine uzisahau kabisa ili utoe mkazo pekee kwa Wizara ya afya, hivyo utasababisha mambo ya kiserikali na mambo ya utendaji katika shughuli za nchi kusimama.

Kwa hivyo naomba tuendelee kukubaliana kwamba Serikali itaelekeza kwa kiwango kikubwa sana na kuweka umuhimu mkubwa sana katika masuala mazima ya afya, lakini vile vile kuona na umuhimu wa sekta nyengine kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, hasa hasa sekta ambazo zitaimarisha uchumi wa nchi yetu kama tunalivyosema mwanzo, ili kujenga nguvu zaidi na kuwezesha uwezo mkubwa zaidi kwa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine la azimio la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub ni Serikali kupitia Wizara ya fedha kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya zinaingizwa zote kwa wakati.

Mheshimiwa tunakwenda na suala la *cash budget* nia yetu ni kuhakikisha kwamba sekta hii inapata msukumo. Ushauri huu tunauchukua lakini utaendana sana na uwezo halisi wa kipato kilichopatikana katika makusanyo ya Serikali ili kusaidia shughuli nzima za Wizara ya Afya kwa nia ile ile ya kusaidia wananchi wetu, na ningependa ielewewe kwamba Serikali siku zote itaendelea kutafuta kila njia na kila mkakati utakaowezesha kutoa huduma bora za afya ili kusaidia sana maslahi ya kujenga afya za watu wetu.

Azimio la tano, Serikali ifanye marekebisho ya mishahara na maslahi ya wataalamu wa afya. Shughuli hii Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza na inafanya kila linalowezekana katika kuhakikisha kwamba maslahi ya wataalamu wetu katika sekta ya afya yanapewa kipaumbele. Kwa hivyo nishauri zuri na tunaendelea nalo kama ambavyo tumeanza vizuri ndani ya Serikali.

Azimio la sita kwamba Wizara ya Elimu na Bodi ya Mikopo Zanzibar kushirikiana na Wizara ya Afya wajielekeze katika mpango wa muda mrefu wa kusomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini. Ni wazo zuri na tunalipokea kadri ya uwezo utakapopatikana katika Bodi ya Mikopo basi jambo hili tutalipa kipaumbele pamoja na kuona kipaumbele vile vile kwa wataalamu wengine muhimu kwa ajili ya kujenga nchi yetu.

La mwisho ni azimio la saba ambalo Serikali iandae mkakati madhubuti na wenye kutekelezeka ndani ya muda mfupi kwa ajili ya kujaribu kuwarejesha nchini wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali, wanaokimbilia sehemu mbali mbali duniani.

Moja ambalo Serikali imefanya katika eneo hili ni suala zima la kuongeza mishahara, kuwaongeza na kuwapa fursa wataalamu wa mambo ya afya katika masomo mbali mbali, hususan katika masomo ya juu na vile vile sasa hivi tunajikita katika kuboresha sekta nzima ya afya, kuanzia kivifaa, kimajengo na mambo mengine muhimu ambayo yatasaidia katika kuimarisha sekta ya afya. Kwa hivyo jambo hili linafanyika na ushauri wake mzuri tutaendelea kuufanya kazi kwa misingi ya kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora nchini.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono pamoja na yale maelezo ambayo nayatoa ili tuone yale yanayowezekana katika maazimio haya yafanyike, na yale ambayo hayawezekani tuyaweke kando, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote niwashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:..... kwa kuwa Mheshimiwa Jaku kidogo amepungukiwa na mavazi katika kuva viyatu, amevaa viyatu vya *sandos* kwa hivyo tunaomba abadilishe viatu ili aweze kujibu hoja zilizobakia Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nina matatizo ya mguu si kawaida yangu mie kuva viatu kama hivi tokea baraza kuanza, kwa hivyo Mheshimiwa Muhammed Aboud Mohammed alijue hilo, naomba kumpa tahadhari kidogo si kawaida yangu nina buti zuri sana Mheshimiwa Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Sawa barua yako tunayo endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru Wajumbe waliochangia hoja hii na ukilinganisha wote waliochangia hoja hii ni wenye majimbo isipokuwa Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed tu. Vile vile nitakuwa sijafanya haki waliokuwa hawakuchangia hoja hii nao niwashukuru. Lakini kuna vitu viwili tofauti kwa aliochangia na waliokuwa hawakuchangia. Waliochangia nawashukuru zaidi na zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nitambue uwepo wa wachangiaji wa hoja hii. Mchangiaji wetu wa mwanzo alikuwa Mhe. Mohamedraza Hassanali Muhamedali wa Jimbo la Uzini, mchangiaji wa pili Mheshimiwa Mahmoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni, mchangiaji wa tatu alikuwa Mhe. Salmin Awadh Salmin muwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Mchangiaji wa nne alikuwa mwana Mapinduzi na muasisi Mhe. Saleh Nassor Juma muwakilishi makini wa Jimbo la Wananchi wa Wawi.

Mchangiaji wa tano alikuwa Mhe. Naibu Waziri vile vile ni muwakilishi wa Jimbo la Kiembe Samaki Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na kwa kumalizia alikuwa Mheshimiwa Muwakilishi Mohammed Aboud Mohammed wa Jimbo la Ikulu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nianze kuzichambua baadhi ya hoja zilizokuwa muhimu na kwanza nianze na Mheshimiwa Mohamedraza Hassanali Muhamedali kwa kunipongeza kuleta hoja hii na ya aina yake, na alichokigusia zaidi ni suala la bajeti.

Suali la bajeti limechangiwa na wajumbe wengi, na bila ya fedha huwezi kufanya lolote tutakuwa tunampigia mbuzi gitaa tu siku zote. Vile vile akazungumzia changamoto za hospitali kuu ya Mnazi mmoja ambayo inategemewa

kuitwa Hospitali ya rufaa kuna changamoto nyingi. Tukianza kuzitaja muda utakuwa hautoshi lakini changamoto zipo nyingi nyingi, pamoja na kitanda kimoja kulala wagonjwa wawili na wengine kutandika chini.

Nije na hoja ya Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni aligusia suala zaidi la maslahi ya daktari; suala hili limechangiwa na wachangiaji wengi. Maslahi ya daktari kwa kweli ni finyu na hayaridhishi kweli kutokana na hali yetu inavyokwenda. Kwa hivyo ipo haja ya Serikali kulipokea mikono miwili hili suala, vyenginevyo itakuwa hali ndio ile ile.

Nije na mchangiaji namba tatu Mheshimiwa Salmin Awadh Salmin muwakilishi wa wananchi wa jimbo la Magomeni alilia sana kuhusu suali lile la bajeti kwa Wizara ya afya kwamba bado ipo haja ya kuongezewa bajeti kwa hali na mali, na kupewa kwa wakati muafaka na ikiwezekana Serikali wapewe wakati ule ule. Mheshimiwa Salmin alisema kuwa bajeti ni ndogo na akapendekeza angalau kwa asilimia kumi kama mfano kwa nchi za SADC kama vile Abuja nafikiri wanapokea asilimi 15 hivi sasa.

Nije na mchangiaji namba nne Mhe. Saleh Nassor Juma muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Wawi kwa kunambia nimechelewa sana mswada huu kuuleta, lakini nimwambie bado sijachelewa nilikuwa ni Mwanagenzi bado ningali nasoma humu ndani. Si kazi rahisi ilikuwa kuja kukurupuka tu kuja kuleta kitu ambacho huna uhakika nacho; kwa hivyo Mheshimiwa Salehe sijachelewa muhimu nia ilikuwa ni nzuri na utekelzaji tu.

Mheshimiwa Saleh aligusa suala la bajeti vile vile kwa kweli wengi wa wajumbe waliochangia waligusa hoja ya bajeti; bajeti Wizara ya afya kwa kweli ni ndogo na ukigusa suala la vipimo, hivi sasa wananchi wetu bado wanapata matatizo kupanda boti kufuata kipimo Dar es Salaam, bado vipimo Mnazi Mmoja haviridhishi kwa muda huu nafikiri hivi juzi tu labda baada ya kupeleka suala Baraza la Wawakilishi nafikiri ndio kipimo kimerekebishwa ambacho kimenunuliwa kwa dola 85,000/, karibu milioni mia moja na ishirini kutoka Oman.

Nije kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, mchango wake mkubwa alioutoa kubwa kuhusu jukumu la Serikali; hili Mhe. Naibu Waziri kuweka kamati hili ni jukumu la Wizara mimi nataka kujitoa, hili watashughulika wenyewe kwa suala la vipimo hivyo.

Mwisho Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed nae nimshukuru sana kwa kuyaona maazimio yote saba niliyoyapitisha hapa na kwa niaba ya Serikali inaonekana imeyachukua na itayafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda niombe tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii tena kwa kutoa majumuisho juu ya hoja yangu. Aidha kwa kuwa wachangiaji wote saba wameonesha nia na dhamiara ya kuunga mkono hoja yangu, naomba niwashukuru sana, kuwajali wananchi wetu. Kwa msingi huo naomba sasa Baraza lako liyapitishe maazimio yote saba kama nilivyopendekeza. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa kiutaratibu kwa kuwa maazimio yapo saba nitasoma moja nitawahoji tukimaliza tutakwenda la pili mpaka tuyamalize; wale wanaunga mkono watanyoosha mikono, na wanaokataa watanyoosha mikono vile vile.

Katibu: Waheshimiwa Wajumbe tunasoma Maazimio yanayotokana na hoja ya Mjumbe kuhusu uimarishaji wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi wa Zanzibar.

Azimio la kwanza kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya kisera yatakayowezesha Serikali kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuwasomesha wataalamu wetu nje ya nchi ili waweze kuwahudumia wananchi badala ya kuchanga fedha nyingi kwa ajili ya kupeleka Wagonjwa nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika: Nawahoji waliokubali azimio namba moja wanyooshe mikono.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kutokana na kanuni za Baraza naomba yale marekebiso kama Meza yako ya makatibu itaweza kuyazingatia, na hapa msemaji mkuu wa Serikali Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais alieleza pale ambapo fedha zitakuwepo za kutosha, au zitakapopatikana; maana hizi fedha wanazopelekewa wagonjwa India sio kama zipo, hazipo lakini zinatafutwa kwa ajili ya *emergency* kwa ajili ya kuwapeleka wale wagonjwa.

Kwa hivyo Azimio namba moja fedha zitakapokuwepo na natumai kwa kila Azimio kuna mambo ambayo Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed alizungumzia kwa upande wa Serikali pamoja na marekebisho yake yawemo, au neno pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mumekubali azimio hilo, waliokataa hakuna, haya tunaendelea la pili.

Katibu: Azimio la pili kwamba mabadiliko haya ya kisera yaendane, kuwa na mkakati wa kusomesha kwa awamu, wataalamu wa fani ambazo zina upungufu hususan katika magonjwa sugu ambayo yanashindikana kutibiwa ndani ya Zanzibar na kuacha kujikita katika kusomesha wataalamu katika fani hizo hilo, ambazo tayari zina wataalamu wa kutosha .

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe azimio la pili limekubaliwa.

Katibu: Azimio la tatu kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya mfumo wa kibajeti kuanzia mwaka 2015/2016 utakaowezesha kupunguza kwa kiwango maalum. Bajeti zinazotengwa katika sekta nyengine ili kuweza kuongeza kiwango cha bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta ya afya nchini, itakayowezesha ununuzi wa vifaa vyta kisasa vya uchunguzi na matibabu pamoja na kusomesha watalam mabingwa wa maradhi mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, azimio hili kama nilivyota maelezo ya awali kwamba bado ziko sekta muhimu zina umuhimu wake, na hivi sasa moja katika eneo la kipaumbele imo na sekta ya afya, kwa hivyo ningeomba kwamba Baraza lako tukufu lione kwamba jitihada zinazochukuliwa na Serikali tuendelee na mfumo wetu uliopo wa kibajeti, na kuweka mkazo katika suala zima la kuimarisha sekta za afya kama inavyota mkazo.

Lakini unaposema kwamba sekta nyengine zipunguziwe kiwango cha fedha wakati nazo vile vile zina mahitaji yake na pia haipatikani fedha ya kutosha kwa ajili ya hilo; nafikiri tuwaachilie wenzetu wa Wizara ya fedha na mfumo wanaoendelea nao umetusaidia sana katika kuendesha shughuli zetu za Serikali.

Vyenginevyo kuingilia sana katika shughuli za utendaji inawezekana kabisa kuleta athari kubwa sana katika suala zima la mgao wa fedha, ambalo matokeo yake inaweza kudumaza sekta nyengine. Kuna umuhimu sana katika kuimarisha sekta ya afya nia ya Serikali kufanya hivyo mipango mbali mbali inachukuliwa kadri ya kuimarisha sekta hiyo. Kwa hivyo naomba azimio hili lituelekeze katika kuhakikisha kwamba pale Serikali itakapokuwa na uwezo iendelee kuongeza uwezo zaidi, lakini mfumo wa sasa uendelee kwa msingi wa kusaidia shughuli zetu zote za Serikali.

Mhe. Naibu Spika: Kwa hivyo waheshimiwa kazi hii imeondoshwa kwa kupunguza kwa kiwango maalum katika sehemu, sekta nyengine hiyo tunaiondoa tunarekebisha kama alivyozungumza Waziri katika Afisi ya Makamo wa pili wa Rais; wanaokubaliana na azimio hilo wanyoshe mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda.

Katibu: Azimio la nne kwamba Serikali kuptitia Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba fedha zinazotengwa katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya zimeingizwa zote kwa wakati ili Wizara ya afya iweze kutimiza wajibu wake kama inavyojipangia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba bajeti yatu na *cash budget*, kadiri ya uwezo wa Serikali nia yetu ni kuingiza fedha kama zinavyotakiwa kwa wakati lakini *kuji-commit* mia kwa wakati mwengine tunachokifanya fedha hazitoshi kiwango hicho na kuna utaratibu maalum wa kugawa mapato, kutohana na makusanyo kwa mwezi naomba utaratibu huo uendelee kutumika ili kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinafanikiwa.

Kwa sababu unaweza kusema hapa unachokikusanya kidogo naomba Mheshimiwa Spika, hili suala la kwamba fedha zinazohitajiwa zote kwa wakati si rahisi na twende na mfumo wetu tulionao wa *cash budget* ambao ndio uliotufikisha hapa tulipofika katika kuendesha shughuli zetu za Serikali, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Kwa hivyo eneo hili linarekebishwa kwamba fedha zinazopatikana ziingizwe kwa wakati, waliokubali. Azimio hilo wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda. Twende azimio la tano.

Katibu: Azimio la tano kwamba Serikali ifanye mabadiliko ya Mshahara na maslahi ya wataalamu wa afya ili kuwapa moyo wataalamu wetu na hivyo waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, lakini pia kuwa na maslahi mazuri yatakayopelekea wataalamu hao kubaki nchini na kuwashudumia wananchi.

Mhe. Naibu Spika: Azimio namba tano wanaounga mkono wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Tunaendelea azimio namba sita.

Katibu: Azimio namba sita kwamba Wizara ya Elimu na Bodi ya Mikopo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wajielekeze katika mpango wa muda mrefu wa kusomesha na kupata wataalamu mabingwa wa maradhi mbali mbali hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika: Azimio namba sita wanaounga mkono wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Tunaendelea azimio la mwisho la saba.

Katibu: Azimio la Saba kwamba Serikali iandae mkakati madhubuti na wenye kutekelezeka ndani ya muda mfupi kwa ajili ya kujaribu kuwarejesha nchini wataalamu na mabingwa wa maradhi mbali mbali waliokimbilia sehemu mbali mbali duniani, kwa sababu mbali mbali ikiwemo na maslahi.

Mhe. Naibu Spika: Azimio namba saba wanaounga mkono wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Kwa hivyo waheshimiwa maazimio yote hayo tutayakabidhi Serikali ili kuyafanya kazi kama vile tulivyokubalina katika Baraza letu hili.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa kuweza kufanya kazi yetu vizuri tangu asubuhi hadi sasa hivi na ushirikiano mzuri mlionipa, nashukuru sana. Kwa hivyo sina tangazo lolote isipokuwa nimeambiwa nisitisize kwamba mazoezi yameanza ya timu yetu lakini Waheshimiwa hawaendi kwenye mazoezi, kwa hivyo naomba sana Waheshimiwa twendeni mazoezini tusije tukafungwa. Baada ya maelezo hayo niahirishe kikao hiki hadi kesho siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi.

(Saa 6.40 mchana Baraza lilahirishwa mpaka tarehe 28/10/2014 Saa 3.00 Asubuhi)